


# Unabii wa Ḥabari za Biblia



Jiwe la Tel Dani linarejea  
'Nyumba ya Daudi'

(9th Century B.C.)

**Ni Nani Mtu wa Uasi? Je Huyu Ndiye  
Mnyama wa kwanza ama wa pili wa  
Ufunuo 13?**

**Amri Kumi na Mtu wa Uasi:  
Je Mtu wa Uasi anakiuka Amri  
Zote Kumi?**

# Unabii wa Habari za Biblia

Katika makala hii:

2. **Kutoka kwa Mhariri: Yote Yanahusu Upendo.** Wakati mambo mengi ni ya muhimu, tusikose kuangalia kwamba Biblia kwa hakika inahusu upendo.
7. **Ni Nani Mtu wa Uasi?** Je Huyu Ndiye Mnyama wa kwanza ama wa pili wa Ufunuo 13?
15. **Amri Kumi na Mtu wa Uasi:** Je Mtu wa Uasi anakiuka Amri Zote Kumi?
20. **Siku Kuu ya Baragumu** Je wajua zaidi kuhusu Siku Kuu?
23. **Je, Mungu Anakuita?** Je, unaweza kueleza?
29. **Kozi ya Biblia: Somo la 12b: Thibitisho la Historia ya Biblia.** Kuna Thibitisho la Historia kwamba Biblia ni ukweli.

Jalada la Nyuma:  
Intaneti na Redio: Hii  
inaonyesha watu mahali  
pa kupata ujumbe wa  
Kanisa la Mungu  
Linaloendelea (CCOG).

Kuhusu Jalada la Mbele:  
Hii picha ilichukuliwa na  
Oren Rozeni wa Jiwe la  
Tel Dani: Hii inazingatiwa  
kuwa ni moja kati ya  
thibitisho la awali lililo  
imara sana, thibitisho  
linalopatikana nje ya  
Biblia, la Mfalme Daudi  
wa Israeli. Sehemu  
nyeupe imeandikwa  
katika lugha ya Kiarama  
(ambayo inafanana na  
Kifanisia) inayosema,  
“Nyumba ya Daudi.”

Unabii wa Habari za  
Biblia inachapishwa na

Kanisa la Mungu  
Linaloendelea (CCOG),  
1036 W. Grande Avenue,  
Grover Beach CA,  
93433.<https://www.ccog.org>

©2017 Kanisa la Mungu  
Linaloendelea (CCOG).  
Imechapishwa  
Marekani. Haki zote  
zimehifadhiwa.

Kunakili makala yote  
ama sehemu yake pasipo  
ruhusa ya kimaandishi  
toka kwa mmiliki  
hairuhusiwi.  
Tunaheshimu haki zako  
hivyo hatutoi, kuuza ama  
kukodisha orodha ya  
mawasiliano yetu.  
Endapo haungependa  
kuupokea gazeti hili,  
wasiliana na ofisi yetu ya

Grover Beach. Maandiko  
yamenukuriwa toka New  
King James version ©  
Thomas Nelson, Inc,  
Publishers, inatumika  
kwa idhini isipokuwa  
pale tu tumeelezwa  
vinginevyo.

Habari za Unabii wa Habari za  
Biblia HUWEZESHWIA KWA  
MICHANGO YENU.

Mhariri Mkuu: Bob Thiel

Makala/Mhariri Msaidizi:  
Joyce Thiel

Mashahihisho: John Hickey;  
SBC Msaidizi wa Kozi: Shirley  
Gestro.

Picha: Picha zote zimetokana  
na familia ya Thiel ama na  
vyanzo vya kijamii kama vile  
Wikipedia ama serikali fulani  
(isipokuwa sifa imetolewa).



## KUTOKA KWA MHARIRI MKUU: BOB THIEL

### Masalio ya Wanafiladelfia: Yote Yanahusu Upendo

Masalio ya Wanafiladelfia ya Kanisa la Mungu yanahusu nini?

Je, ni kundi tu ama shirika la wanaodhani wanafuata sheria zinazostahili?

Kwa muda wa masaa 25 ya uundaji wa Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG), niliandika kwamba kwa hakika yote yanahusu upendo-maisha ya "kutoa."

Wakati sheria ni muhimu (Yohana 14:15; Mathayo 23:23), ni nini muhimu zaidi?

Kulingana na Yesu, mitume, na hayati Herbert W. Armstrong, na Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG), upendo ndio wa muhimu sana.

Mpango wa Mungu unahusu upendo. Kumbuka alivyosema Yesu:

16 Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ila kila mtu amwaniye asipotee, bali awe na uzima wa milele. 17 Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. (Yohana 3:16-17)

Lakini siye Mungu tu anafaa kupenda. Kumbuka baadhi ya aliyorekodi Marko:

28 Na mmojawapo wa waandishi akafika, akawasikia wakisemezana naye, akatambua ya kuwa amewajibu vema, akamwuliza,

Katika amri zote ni ipi iliyo ya kwanza? 29 Yesu akamjibu, Ya kwanza ndiyo hii, Sikia Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja, 30 nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote. 31 Na ya pili ndiyo hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri iliyo kuu kuliko hizi. 32 Yule mwandishi akamwambia, Hakika, Mwalimu, ume sema vema ya kwamba Mungu ni mmoja, wala hakuna mwingine ila yeye; 33 na kumpenda yeye kwa moyo wote, na kwa ufahamu wote, na kwa nguvu zote, na kumpenda jirani kama nafsi yako, kwafaa kuliko sadaka nzima ya kuteketezwa na dhabihu zote pia. 34 Naye Yesu alipoona kwamba amejibu kwa busara, alimwambia, wewe hu mbali na ufalme wa Mungu. Wala hakuthubutu mtu kumsaili neno tena tokea hapo. (Marko 12:28-34)

Umuhimu wa upendo umethibitishwa na wengi katika Agano Jipy. Kumbuka maelezo haya kutoka kwa Mtume Paulo:

13 Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo, haya matatu; katika hayo lililo kuu ni upendo. (1 Wakorintho 13:13)

Kumbuka mafungu mengine yaliyoandikwa na Mtume Yohana:

7 Wapenzi, na mpandise; kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu, na kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu. 8 Yeye asiyependa hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni upendo. 9 Katika hili pendo la Mungu lililonekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni, ili

tupate uzima kwa yeye.10 Hili ndilo pendo,si kwamba sisi tulimpenda Mungu,bali kwamba yeye alitupenda sisi,akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu. 11 Wapenzi ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi,imetupasa na sisi kupendana.12 Hakuna mtu aliywona Mungu wakati wo wote.Tukipendana Mungu hukaa ndani yetu,na pendo lake limekamilika ndani yetu.13 Katika hili tunafahamu ya kuwa tunakaa ndani yake,naye ndani yetu,kwa kuwa ametushirikisha Roho wake.14 Na sisi tumeona na kushuhudia ya kuwa Baba amemtuma Mwana kuwa Mwokozi wa ulimwengu.15 Kila akiriye ya kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu,Mungu hukaa ndani yake,naye ndani ya Mungu.16 Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi,na kuliamini.Mungu ni upendo,naye akaaye katika pendo,hukaa ndani ya Mungu,na Mungu hukaa ndani yake.17 Katika hili pendo limekamilishwa kwetu,ili tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu;kwa kuwa,kama yeye alivyo,ndivyo tulivyo sisi ulimwenguni humu.18 Katika pendo hamna hofu;lakini pendo lililo kamili huitupa nije hofu;kwa maana hofu ina adhabu;na mwenye hofu hakukamilishwa katika pendo.19 Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza.20 Mtu akisema,Nampenda Mungu,naye anamchukia ndugu yake;ni mwongo;kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona,hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona.21 Na amri hii tumepewa na yeye,ya kwamba yeye ampenday Mungu,ampende na ndugu yake. (Yohana 4:7-21)

1 Kila mtu aaminiye kwamba Yesu ni Kristo amezaliwa na Mungu.Na kila mtu ampendaye mwenye kuzaa, ampenda hata yeye aliyezaliwa na yeye.2 Katika hili twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu, tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake.3 Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito. (1 Yohana 5:1-3)

Yafuatayo yanatoka kwa kitabu cha Herbert W. Armstrong kiitwacho *Ajabu ya Kudumu:*

Dini ya Ukweli-Ukweli wa Mungu unaowezeshwa na upendo wa Mungu unaotolewa na Roho Mtakatifu...FURAHA YA KIFANI ya kumjua Mungu na Yesu Kristo-ya kujua UKWELI-na uchangamfu wa UPENDO mtakatifu!...

“Naye neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, (nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee, atokaye kwa Baba,) ameja neema na kweli.”...Na sura ya Yesu ilikuwaje? Ilikuwa kama ya mwanadamu, kwa sababu alikuwa pia Mwana wa adamu...

Yaliyo muhimu kuliko yote hata hivyo ni asili ya Mungu-TABIA yake ni ipi? Hakuna hawezaye kumjua Mungu asipojua TABIA yake!

TABIA ya Mungu Baba na Mwanawe Kristo ni ile ya utakatifu wa kiroho, wa haki na utimilifu kamili.

Tabia hio inaweza kujumuishwa kwa neno moja UPENDO, ambalo linafafanuliwa kama uhusiano unaobubujika na ya upendo. Ni njia ya kutoa, kuhudumia, kusaidia, kugawa lakini siyo njia ya “KUPATA.”

Ni njia isiyo na tamaa, uchoyo, ubatili na ubinafsi, mashindano, ugomvi, machafuko na uharibifu, wivu, chuki na uchungu...

Amri ya Mungu ni ya Kiroho na inaweza kujumuishwa katika neno moja rahisi lakini labeba kila kitu-upendo. Amri yake kwa kuongoza mwenendo wa binadamu imegawanywa katika amri mbili kuu, upendo kwa Mungu na upendo kwa jirani. Hizi, kwa zamani, zimegawanywa katika amri 10. Yesu alitukaza amri hii kwa kuonyesha jinsi kanuni zake zimepanuka kwa kushika hakika kila uwezekano wa machafuko ya wanadamu...

Ujue kwamba serikali ya Mungu imeundwa kwenye msingi ya SHERIA ya Mungu, ambayo ni njia ya UPENDO ububujikao, ushirikiano, uhusiano mwema kwa wanaotawaliwa...

Kuelewa kwa kina AMRI za Mungu (njia yake ya maisha) kunawezeshwa na Roho Mtakatifu. Lakini Amri za Mungu inahitaji utekelezaji na utendaji, na UPENDO ndio utimilifu wa amri ya Mungu (Warumi 13:10), na inaweza kukamilishwa na upendo kutoka kwa Mungu pekee (Warumi 5:5) ...

Katika mapigo Mungu alifanya dhidi ya Wamisri, Mungu aligeuza miungu yao na vifaa vyao vya kuabudu dhidi yao kuwaonyesha kwamba hivyo havikuwa miungu. Hata mapigo yalitumwa katika UPENDO kwa Wamisri...

Mkristo lazima akue na kuendelea katika neema, maarifa ya kiroho na tabia ya kiungu... akionyesha upendo mwangi ama uhusiano mwema kwa wengine...

Fundisho la kimsingi, imani NA MAFUNDISHO YA Kanisa la ukweli la Mungu basi yamejengwa kwenye haki na utiifu wa amri ya Mungu. Amri hiyo ni UPENDO. Lakini sio upendo wa binadamu. Upendo wa binadamu hauwezi kupanda juu ya kiwango cha ubiniasi wake. Ni lazima uwe ni "pendo la Mungu...lililominwa katika miyo yetu na Roho (Mtakatifu)" (Warumi 5:5). Waisraeli wa kale hawangeweza kuitii sheria ya Mungu-wangeitunza sheria kulingana na adhabu kali ya sheria. Lakini kwa vile upendo ndio utimilifu wa sheria

na wao walikuwa na upendo wa ubiniasi, hawangeweza kuitunza sheria kulingana na roho-kwa sababu Roho Mtakatifu bado hakuwa amekuja.

Fundisho hili basi linajumuisha "matunda yote ya Roho Mtakatifu"-upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, imani, upole, kiasi, nk.

Watu watageuka kutoka kwa njia ya "kupata" waende kwenye njia ya "kutoa"-njia ya Mungu ya Upendo.

USTAARABU MPYA sasa utakamata dunia!

Kuutangaza huo ustaarabu mpya kwamba unakuja na utakuwa wa upendo ndio inahusu sehemu kubwa ya injili ya ukweli ya ufalme.

Mtume Paulo katika mahali fulani alitaja sehemu nyingine kama "habari njema ya neema ya Mungu" (Matendo 20:24).

Mtume Paulo pia aliandika:

1 Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama siyo upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. 2 Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, si kitu mimi. 3 Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidi kitu. 4 Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hausudu; upendo hautakabari; haujivuni; 5 haukosi kuwa na adabu, hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; 6 haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; 7 huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahimili yote. 8 Upendo haupungui neno wakati wo wote; bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo

lugha,zitakoma;yakiwapo maarifa yatabatilika.9 Kwa maana tunafahamu kwa sehemu;10 lakini ijapo ile iliyo kamili,iliyo kwa sehemu itabatilika.11 Nilipokuwa mtoto mchanga,nalisema kama mtoto mchanga,nalifahamu kama mtoto mchanga,nalifikiri kama mtoto mchanga;tokea hapo nilipokuwa mtu mzima,nimeyabatilisha mambo ya kitoto.12 Maana wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo;wakati ule tutaona uso kwa uso;wakati wa sasa nafahamu kwa sehemu;wakati ule nitajua sana kama mimi nami ninavyojuliwa sana.13 Basi,sasa inadumu imani,tumaini,upendo,haya matatu;na katika hayo lililo kuu ni upendo.(1 Wakorintho 13:1-13)

### Kwa Nini Kuna Masalio ya Wafiladelfia?

Kanisa la Laodikia ndilo kanisa la mwisho lililotajwa katika kitabu cha Ufunuo (Ufunuo 3:14-22). Kama kanisa la mwisho, litabaki kutawala sana katika nyakati za mwisho. Neno “Laodikia” linaweza kumaanisha “watu wanatawala,” “hukumu ya watu,” ama “watu wanaamua.”

Yesu alilaumu kazi ya Walaodikia.

Laodikia inahusishwa na kukana uongozi ambao umekubaliwa na Wafiladelfia-Kuwakubali viongozi wa kanisa kulingana na maandiko (1 Wakorintho 12:28;Waefeso 4:11-16),pamoja na mtazamo wa kawaida ya uvuguvugu.Kwa hivyo uongozi ndio tofauti kubwa kati ya Filadelfia na Laodikia.Laodikia wanatilia mkazo ubinafsi (wao wenyewe ama kwa viongozi badala ya kuutangaza ukweli wote pamoja na Injili),hivyo wanachakachua hata ukweli-na hivyo “wanakemewa na kurudiwa ” na kushauriwa “wanunue Kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto” (Ufunuo 3:18-19).

Kwa sababu Laodikia wamekuwa wengi katika nyakati za mwisho, Wafiladelfia

hawawezi basi kuwa wengi kwa idadi. Hata hivyo, sehemu ya Filadelfia lazima iwepo bado.

Twajua haya kwa sababu Yesu aliwaambia Wafiladelfia: “Kwa kuwa umelishika neno la subira yangu, mimi nami nitakulinda, utoke katika saa ya kuharibiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote, kuwajaribu wakaa juu ya nchi.11 Naja upesi!” (Ufunuo 3:10-11). Wanafiladelphia, wale masalio ya Filadelfia wa Kanisa la Mungu, ndio wameahidiwa ulinzi! Wafiladelfia “wamepewa mabawa mawili ya tai yule mkubwa, ili aruke, aende zake nyikani hata mahali pake, hapo alishwapo kwa wakati na nyakati na nusu ya wakati, mbali na nyoka huyo” (Ufunuo 12:14).

Zaidi ya hayo, kwa vile Yesu anasifu kazi ya Kanisa la Filadelfia, na ushahidi mkuu wa kuhubiri habari njema ya Ufalme wa Mungu lazima ifanywe ili ifyatulie mwisho (Mathayo 24:14), ni lazima masalio ya Wafiladelfia ndio wafanye kazi hiyo.

1 Upendano wa ndugu na udumu.  
(Waebrania 13:1)

Neno la Kigiriki lifasiriwayo kama “upendano wa ndugu” ni neno Filadelfia.Mwandishi wa kitabu cha Waebbrania ni kama alitiwa msukumo kupasa dhana mbili:

Kwamba upendo unahitajika kuendelea mionganoni mwa wale wanaoamini kwamba ni Wakristo.

Na pengine kwamba Filadelfia yenye we inahitajika kuendelea, na inaweza kuendelea, kwa sababu ya msisitizo wa upendo.

Ni muhimu kwa wote kugundua kwamba licha ya dosari ya Wakristo, pamoja na sisitulio wa masalio ya Filadelfia, yote yanahusu upendo huo ambao ndio njia ya Mungu ya maisha na Ufalme.Na kuutangaza huo ujumbe wa upendo na njia zote za Mungu ndiyo Kanisa la Mungu Linaloendelea wanataka kufanya.

Ujumbe huu ndio ulikuwa mada katika kipindi cha kwanza cha Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG). Ulikuwa pia ujumbe wa kwanza nilitoa nchini Kenya nilipowatembelea mnamo 2014 na pia mwaka wa 2017.

Kamusi cha kina cha Strong inaonyesha kwamba Filadelfia linamaanisha “upendano wa ndugu” ama “uzoefu wa ndugu.”

Wakati Yesu alitumia neno *phileo* kwa Simoni Petro (linalotafsiriwa kama “upendo”), Petro angefanya nini kuonyesha aina hiyo ya upendo? Angefanya kazi.

17 Akamwambia mara ya tatu, Simoni wa Yohana, wanipenda? Petro alihuzunika kwa vile alivyomwambia mara ya tatu, Wanipenda? Akamwambia, Bwana, wewe wajua yote; wewe umetambua ya kuwa nakupenda. Yesu akamwambia, Lisha kondoo zangu” (Yohana 21:17).

Tabia ya Wafiladelfia ni kwamba wana upendano wa ndungu na wanaweza kujitoa kwa kufanya hivyo. Wakati wengine wanaweza kusema kwamba hili linamaanisha wale tu walioko kanisani, hili haliendi na Mathayo 28:19-20 na vile vile maneno ya Yesu katika Yohana 10:16: “Na kondoo wengine ninao amba si wa zizi hili; na hao nao imenipasa kuwaleta; na sauti yangu wataisikia; kasha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja.”

Wafiladelfia wanawapenda wengine, sio wao pekee yake. Kama vile Herbert W. Armstrong aliandika:

Enzi hii ya Kanisa ilifaa izae tunda (Ajabu ya Kudumu, uk.290).

Dini ya ukweli-Ukweli wa Mungu unaowezeshwa na upendo wa Mungu unaotiwa na Roho Mtakatifu-FURAHA USIOWEZA KUNENWA wa kumjua Mungu na Yesu Kristo-wa Kuujua UKWELI-na msisimko

wa UPENDO wa Mungu ulio takatifu! (Ajabu ya Kudumu).

Kama vile Yesu alivyofundisha: “Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake, ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili, huyu ataisalimisha” (Marko 8:35). Wafiladelfia watatoa yote walio nayo ili wahubiri Injili.

Wafiladelfia wana ”nguvu kidogo, wamelimunza neno la Mungu, wala hawakulikana jina lake” (Ufunuo 3:8). Sio sehemu ya Kanisa lenye nguvu (ama kanisa kubwa kwa mtazamo wa dunia).

Wametunza neno la Mungu bila kulichakachua. Hawajawahi kukataa mamlaka ya Yesu (kama vile Strong inafafanua neno lililotafsiriwa “jina”).

Wafiladelfia wanakubali kwamba “Kristo ndiye kichwa cha Kanisa” (Waefeso 5:23), na wanakubali mamlaka ilioko ndani ya Kanisa:

11 Naye alitoa wengine kuwa mitume,na wengine kuwa manabii;na wengine kuwa wainjilisti na wengine wachungaji na waalimu;12 kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu,hata kazi ya huduma itendeke,hata mwili wa Kristo ujengwe;13 hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu,hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo;14 ili tusiwe tena watoto wachanga,tukitupwa huku na huku,na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu,kwa hila ya watu,kwa ujanja,tukizifuata njia za udnanganyifu.15 Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeche kichwa,Kristo (Waefeso 4:11-15).

Filadelfia wamejiandaa na wanaweza kuhubiria ulimwengu mpaka mwisho ufike, kwa sababu watakuwepo hadi mwisho

ufike. Wafiladelfia wana upendo wa Mungu kwa jirani yao kwa hali ya kuhubiri injili.

Pia watasaidia kwa kazi ya matayarisho ya kazi fupi ambayo Mungu ataiakamilisha (Warumi 9:28).

Ni wale wanaojitolea kabisa katika Kanisa la ukweli la Ukristo ndio watakaomiliza awamu ya mwisho ya kazi kabla ya (Mathayo 24:14) na wakati wa (Ufunuo 11:3-14) Dhiki Kuu na Siku ya Bwana-na awamu ya mwisho pia itahusu kupambana na muungano wa madhehebu ambaou utachipuka (Ufunuo 13:4,8;14:9-13)-na hii ndiyo Kanisa la Mungu Linaloendelea linafanya.

Ingawa watu wengi hawaelewi, masalio ya ukweli ya Filadelfia yanahu upendo. Upendo kwa Mungu, upendo kwa jirani, na kuumiliki upendo wa hakika na ukweli.

(Hii ni miongoni mwa mada niliyotoa wakati tulikuwa na kongamano la viongozi wa Afrika jijini Nairobi, Kenya mnamo Februari 2017).

## Ni Nani Mtu wa Kuasi wa 2 Wathesalonike 2?



*Ufasiri wa msani wa Ujerumani wa mtu wa uasi, 1948.*

Na Bob Thiel  
Mtume Paulo aliandika yafuatayo kuhusu mtu wa uasi, mwana wa uharibifu, katika 2 Wathesalonike 2:

1Basi,ndugu ,tunakusihini,kwa habari ya kuja kwake Bwana wake Yesu Kristo,na kukusanyika kwetu mbele zake,2 kwamba msifadhaishwe upesi hata kuiacha nia yenu,wala msisitushwe,kwa roho wala kwa neno,wala kwa waraka unaodhaniwa kuwa ni wetu,kana kwamba siku ya Bwana imekwisha kuwapo.3 Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yote;maana haiji,usipokuwa kwanza ule ukengeufu;akafunuliwa Yule mtu wa kuasi,mwana wa uharibifu;4 yule mpingamizi,ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa;hata mwenye kuketi katika hekalu la Mungu,akijionyesha nafsi yake kana kwamba ye ye ndiye Mungu.5 Je! Hamkumbuki ya kuwa wakati nilikuwapo pamoja nanyi naliwaambieni hayo? 6 Na sasa lizulialo mwalijua,yule apate kufunuliwa wakati wake.7 Maana ile siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi;lakini yupo azuiaye sasa,hata atakapoondolewa.8 Hapo ndipo atakapofunuliwa yule asi,ambaye Bwana Yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa chake,na kuwaangamiza kwa ufunuo wa kuwapo kwake;9 yule ambaye kuja kwake ni kwa

mfano wa kutenda kwake  
Shetani,kwa uwezo wote,na ishara  
na ajabu za uongo;10 na katika  
madanganyo yote ya udhalimu kwa  
hao wanaopotea;kwa sababu  
hawakukubali kuipenda ile  
kweli,wapate kuokolewa.11 Kwa  
hiyo Mungu awaletea nguvu ya  
upotevu,wauamini uongo;12 ili  
wahukumiwe wote ambao  
hawakuiamini kweli,bali walikuwa  
wakijifurahisha katika udhalimu.(2  
Wathesalonike 2:1-12)

Huyu mtu wa mwisho wa dhambi ndiye  
atakuwa mbele kwa kujihusisha na miujiza  
ya kiajabu ambayo itaathiri ulimwengu  
mzima.

Huyu mtu wa kuasi ni nani?

Wengine wanafundisha mtu wa dhambi ni  
Mnyama wa pili wa Ufunuo 13. Wengine  
wanasema ni Mnyama wa kwanza. Ni nani  
huyu kwa hakika?

### Tutazame Danieli na Ufunuo

Kumbuka kwamba maelezo ya Mfalme wa  
Kaskazini katika Danieli yanakaribia sana  
maelezo ya mtu wa uharibifu:

36 Naye mfalme atafanya kama  
apendavyo;naye atajitokuza na  
kujiadhimisha juu ya kila  
mungu,naye atanena maneno ya  
ajabu juu ya Mungu wa  
miungu,naye atafanikiwa mpaka  
ghadhabu itakapotimia;maana  
yaliyokusudiwa yatafanyika.37 Wala  
haitajali miungu ya baba zake;wala  
ye ye aliyetamaniwa na  
wanawake;wala hatmjali mungu  
awaye yote;maana atajitokuza  
mwenyewe juu ya wote.38 Lakini  
katika mahali pake atamheshimu  
mungu wa ngome;na mungu  
ambaye baba zake hawakumjua  
atamheshimu,kwa dhahabu,na  
fedha,na vito vyta thamani,na vitu  
vipendezavyo. (Danieli 11:36-38)

Linalosemwa na Danieli 11:36 na 2  
Wathesalonike 2:3-4 kuhusu mtu huyu  
linafanana-huyu ni mtu mmoja.

Kumbuka pia kwamba Mfalme wa Kaskazini  
anajitokuza juu ya miungu yote. Hiyo ni  
pamoja na mungu wa ngome, ambayo (vile  
nilivyopendekeza hapo awali) ni mungu wa  
Katoliki wa Kirumi.Na huyu pia anaweza  
kuwa mnyama mwenye pembe mbili wa  
Ufunuo 13.

Biblia inaonyesha kwamba Mnyama wa  
kwanza ataabudiwa na kwamba Mnyama  
wa pili (anayetwa “Mnyama mwingine  
hapa chini”) anafanya ulimwengu  
kumwabudu Mnyama wa kwanza:

1 Kisha nikaona mnyama akitoka  
katika bahari...3 ...Nikaona kimoja  
cha vichwa vyake kana kwamba  
kimetiwa jeraha la mauti,na pigo  
lake la mauti likapona,na Dunia  
yote ikamstaajabia mnyama yule.4  
Wakamsujudu yule joka kwa sababu  
alimpa huyo mnyama uwezo  
wake;nao wakamsujudu yule  
mnyama wakisema,Ni nani  
afananaye na mnyama huyu?...7  
Tena akapewa kufanya vita na  
watakatifu na kuwashinda,**akapewa**  
**uwezo** juu ya kila kabilia na jamaa  
na lugha na taifa.**8 Na watu wote**  
**wakaao** juu ya nchi  
**watamsujudu**,kila ambaye jina  
lake halikuandikwa katika kitabu  
cha uzima cha Mwana  
Kondoo,aliyechinjwa tangu  
kuwekwa misingi ya dunia...11Kisha  
nikaona mnyama  
mwingine,akipanda juu kutoka  
katika nchi;naye alikuwa na pembe  
mbili mfano wa Mwana-  
Kondoo,akanena kama joka.12 Naye  
atumia uwezo wote wa mnyama  
yule wa kwanza mbele yake.Naye  
aifanya dunia na wote wakaao  
ndani yake wamsujudie mnyama wa  
kwanza,ambaye jeraha yake ya  
mauti lilipona.(Ufunuo  
13:1,3,4,7-8,11-12)

Kwa vile Mtu wa kuasi anajitukuza juu ya kila kiitwacho Mungu (2 Wathesalonike 2:3-4) na mnyama wa pili anasababisha ulimwengu kusujudu, siyo kumsujudu lakini kumsujudia mnyama wa kwanza (Ufunuo 13:11-12), mtu wa kuasi lazima awe ni Mnyama wa kwanza.

Kumbuka kwamba mnyama mwenye pembe mbili (ambaye ni nabii wa uwongo, Ufunuo 19:20) anasababisha watu kumsujudu mnyama wa kwanza, mnyama aliye na pembe kumi (na ishara zinazofuata-anazofanya mbele ya MNYAMA WA KWANZA-2 Wathesalonike 2:9-10). Kwa hivyo mnyama aliye na pembe mbili hajitukuzi mbele ya kila kitu kiitwacho mungu kwa sababu ana watu wanaomsujudu mnyama aliye na pembe kumi ambaye anakufuru, kwa sababu ni Mfalme wa Kaskazini ambaye anakufuru (Danieli 11:36-40). Na ni mnyama aliye na pembe kumi ambaye amepewa "mamlaka mkuu," sio mnyama aliye na pembe mbili.

Hakuna andiko ambalo linataja kwamba mnyama wa pili anaabudiwa vile mnyama wa kwanza anafanyiwa. Nabii wa uwongo anaendeleza ibada ya uwongo, kinyume na kuwa kifaa chake yeye mwenyewe. Wakati Papa kwa muda mrefu wamefanya watu kuwapigia magoti mbele yao, sijapata maandiko yoyote ambayo yanaonyesha kwamba nabii wa uwongo mwenyewe anajaribu kujifanya kifaa cha kuabudiwa.

Agano la Kale pia linakubali hivyo.  
Kumbuka pia alichoandika Danieli:

24 Na habari za zile pembe kumi, katika ufalme huo wataondoka wafalme kumi; na mwingine ataondoka baada ya hao wa kwanza, naye atwashusha wafalme watatu. 25 Naye atanena maneno kinyume chake Aliye juu, naye atawadhoofisha watakatifu wake Aliye juu; naye ataazimu kubadili majira na sheria; nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati, na

nyakati mbili, na nusu wakati (Danieli 7:24-25).

Ni mnyama aliye na pembe kumi anayenena maneno ya makufuru dhidi ya Mungu, yeye ndiye anajitukuza mbele ya Mungu (2 Wathesalonike 2:4).

Pia kumbuka kwamba katika Biblia, watu wameonywa dhidi ya kumwabudu yule mnyama wa kwanza:

9 Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, 10 yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo (Ufunuo 14:9-10).

2 Akaenda huyo wa kwanza, akakimimina kitasa chake juu ya nchi; pakawa na jipu baya, bovu, juu ya wale watu wenye chapa ya huyo mnyama, na wale wenye kuisujudia sanamu yake... 10 Na huyo wa tano akakimimina kitasa chake juu ya kiti cha enzi cha Yule mnyama; ufalme wake ukatiwa giza; wakatafunu ndimi zao kwa sababu ya maumivu (Ufunuo 16:2,10).

Hata kama sanamu hii inahusiana na kanisa la Katoliki (ambayo kwa kiwango fulani inahusu kanisa hilo), kumbuka kwamba ni mnyama na sanamu YAKE na ufalme WAKE ambao wanaabudu kinyume cha Mungu kando na nabii wa uwongo. Mnyama yuko na mamlaka juu ya nabii wa uwongo na yeye ndiye anajitukuza juu ya kila kiitwacho Mungu.

Ikiwa tutaiacha Biblia itoe ufanuzi yenyewe, inapendekeza, kwamba maelezo katika 2 Wathesalonike 2:3-4 yanakaribia sana na mnyama wa kwanza, Mfalme wa Kaskazini, na siyo mnyama wa pili ambaye ni nabii wa uwongo.

Kumbuka kwamba mnyama wa kwanza pia anatimiza yafuatayo:

15 Kisha akaniambia, Yale maji uliyoyaona, hapo aketipo yule kahaba, ni jamaa na makutano na mataifa na lugha. 16 Na zile pembe kumi ulizoziona, na huyo mnyama, hao watamchukia yule kahaba, nao watamfanya kuwa mkiwa na uchi, watamla nyama yake, watamteketeza kabisa kwa moto. 17 Maana Mungu ametia miyoni mwao kufanya shauri lake, na kufanya shauri moja, na kumpa yule mnyama ufalme wao hata maneno ya Mungu yatimizwe. 18 Na yule mwanamke uliyemwona, ni mji ule mkubwa, wenye ufalme juu ya wafalme wa nchi. (Ufunuo 17:15-18)

Kumbuka kwamba kahaba (Kanisa la Ekumeni ya Rumi) atamezwa wakati huu. Hii ni njia nyingine ambapo mnyama wa kwanza, mnyama aliye na pembe kumi hazingatii hamu ya wanawake vile Danieli 11:37 inataja (na kanisa la kahaba linaloashiria mwanamke katika Ufunuo 17) na anajitkuza juu ya chochote kiitwacho mungu.

Uharibifu wa kahaba pia inaonyesha mtu wa uasi, mwana wa uharibifu katika 2 Wathesalonike 2, siye nabii wa uongo, lakini mnyama mwenye pembe kumi, na yeye na wanaomwunga mkono wana nguvu na wanatenda badala yake.

Hata hivyo, kwa vile nabii wa uongo bado anaishi katika hatua hii (Ufunuo 19:20), anaonekana mateka ya mnyama aliye na pembe kumi ama kwamba amelisaliti kanisa lake. Lakini nadhani kwamba atafanya hiyo ya mwisho (kwa vile mnyama

wa pili anaendeleza kuabudu kwa mnyama wa kwanza kulingana na Ufunuo 13:12)-ana njama katika kumsaliti Kanisa la Rumi-ambayo ni sababu inayonifanya nifundishe kwamba nabii wa uongo ni aina ya mpinga papa.

### Ishara zitamwandama Mnyama

Shida moja kubwa ya watu wengi ni kwamba hawaoni "mtu wa dhambi/kuasi" kama Mfalme wa Kaskazini (Mnyama wa Kwanza) badala ya Nabii ya Uongo, kwa sababu wanaonekana hawaunganishi "miujiza na ISHARA" kwake LAKINI...Ufunuo 16:13-14 inaonyesha uhusiano kamilii:

13 Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura; zikitoka katika kinywa cha yule joka, na katika kinywa cha yule mnyama, na katika kinywa cha yule nabii wa uongo. 14 Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi.

Tena kumbuka 2 Wathesalonike 2:9:

9 yule ambaye kuja kwake ni kwa mfano wa kutenda kwake Shetani, kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo,

Sasa sio kwamba tuna 2 Wathesalonike 2:9 pekee inayoonyesha ishara zitamwandama "mtu wa kuasi" lakini pia Ufunuo 16:13-14 inaonyesha wazi kwamba MNYAMA kwa kawaiida atafanya ISHARA pia.

### Mtu wa Uasi pia anaitwa Mwana wa Uharibifu

Katika 2 Wathesalonike 2:3 mtu wa kuasi pia anaitwa mwana wa uharibifu.

Pengine inafaa ikumbukwe kwamba neno uharibifu limetajwa mara ngapi (Strong's#684) katika kitabu cha Ufunuo katika mafungu yafuatayo:

7 Na yule malaika akaniambia,  
Kwani kustaajabu? Nitakuambia siri  
ya mwanamke huyu, na ya mnyama  
huyu amchukuaye, mwenye vile  
vichwa saba na zile pembe kumi.8  
Yule mnyama uliyemwona  
alikuwako, naye hayuko, naye yu  
tayari kupanda kutoka kuzimu na  
kwenda kwenye uharibifu. (Ufunuo  
17:7-8)

11 Na Yule mnyama aliyekuwako  
naye hayuko, yeye ndiye wa nane,  
naye ni mmoja wa wale saba, naye  
aenenda kwenye uharibifu. (Ufunuo  
17:11)

Wakati yaliyo juu si thibitisho kamili  
kwamba mnyama mwenye pembe kumi ni  
mwana wa uharibifu, inaonekana inaunga  
mkono dhana hiyo. Mistari hiyo katika  
Ufunuo 17 hasa inaunga mnyama wa bahari  
na uharibifu.

Basi Biblia pia inafundisha kwamba Yuda  
Iskariote alikuwa ‘mwana wa uharibifu:’

12 Nilipokuwapo pamoja nao, mimi  
naliwalinda kwa jina lako ulilonipa,  
nikawatunza; wala hapana  
mmojawapo wao aliyepotea, ila  
yule mwana wa upotetu, ili andiko  
litimie. (Yohana 17:12)

1 Alipokwisha kusema hayo, Yesu  
alitoka pamoja na wanafunzi wake  
kwenda ng'ambo ya kijito Kedroni,  
palikuwapo bustani; akaingia yeye  
na wanafunzi wake.2 Naye Yuda,  
yule aliyetaka kumsaliti, alipajua  
mahali pale; kwa sababu Yesu  
alikuwa akienda huko mara nyingi  
pamoja na wanafunzi wake.  
(Yohana 18:1-2)

Wakati Yuda kwa muda alifikiri kwamba  
alikuwa mfuasi wa Yesu, alikuwa mwongo  
na akamsaliti.

Pia, Mfalme wa Kaskazini, Washuru katika  
Isaya 10, hawatafikiria anamaanisha

kuharibu, lakini iko katika moyo wake  
kufanya hivyo:

5 Ole wako Ashuru! Fimbo ya hasira  
yangu, ambaye gongo lililo mkononi  
mwake ni ghadhabu yangu.6  
Nitamtuma juu ya taifa lenye  
kukufuru, nitampa maagizo juu ya  
watu wa ghadhabu yangu, ateke  
nyara, na kuchukua mateka, na  
kuwakanyaga kama matope ya  
njiani.7 Lakini hivyo sivyo  
akusudiavyo mwenyewe, wala sivyo  
moye wake uwazavyo; maana  
katika moyo wake akusudia  
kuharibu, na kukatilia mbali  
mataifa, wala si mataifa machache.  
8 Maana asema, Je! Wakuu wangu  
si wote wafalme? 9 Je! Kalno si  
kama Karkemishi? Hamathi si kama  
Arpadi? Samaria si kama Dameski?  
10 Kama vile mkono wangu  
ulivyofikilia falme za sanamu,  
ambazo sanamu zao za kuchongwa  
zilikuwa bora kuliko sanamu za  
Yerusalem na za Samaria 11 je!  
Sitauenda Yerusalem na sanamu  
zake vile vile kama nilivyoutenda  
Samaria na sanamu zake?” (Isaya  
10:5-11)

Zaidi ya hayo, Biblia inaonyesha kwamba  
Yuda Iskariote alitumia njama ya  
kudanganya kwa kuiba:

4 Basi Yuda Iskariote.mmojawapo  
wa wanafunzi wake, ambaye ndiye  
atakaye kumsaliti, akasema,5  
Mbona marhamu hii haikuuzwa kwa  
dinari mia tatu, wakapewa maskini?  
6 Naye alisema hayo, si kwa  
kuwahurumia maskini; bali kwa  
mwivi, naye ndiye aliyeshika  
mfuko, akavichukua vilivyotiwa  
humo. (Yohana 12:4-6)

Bibli pia inasema kwamba Mfalme wa  
Kaskazini atatumia njama ya udanganyifu  
kupata nguvu:

21 Kisha badala yake atasimama  
mmoja, mtu astahiliye

kudharauliwa, ambaye hawakumpa heshima ya ufalme; naye atakuja wakati wa amani, naye ataupata ufalme kwa kujipendekeza.22 Na wale wenye silaha mfano wa gharika watagharikishwa mbele yake, na kuvunjika, naam, mkuu wa maagano pia. (Danieli 11:21-22)

34 Basi watakapoanguka, watasaidiwa kwa msaada kidogo; lakini wengi wataambatana nao kwa maneno ya kujipendekeza.35 Na baadhi yao wenye hekima wataanguka, ili kuwatakasa, na kuwasafisha, na kuwafanya weupe, hata wakati wa mwisho; kwa maana ni kwa wakati ulioamriwa, ambao haujaja. (Danieli 11:34-35)

23Na wakati wa mwisho wa ufalme wao, wakosoa watakapotimia, mfalme mwenye uso mkali, afahamuye mafumbo, atasimama... 25 Na kwa mashauri yake atafanikisha hila mkononi mwake; (Danieli 8:23,25)

Biblia inaonyesha kwamba Yuda, ambaye alikuwa ‘mwana wa uharibifu’ aliyemsaliti Yesu na Mfalme wa Kaskazini, ‘mwana wa uharibifu’ ambaye atausaliti ulimwengu wote walitumia mbinu za uongo. Biblia inaonyesha ya kwamba wote wanajaribu kutumia maneno ya uwongo ili wasitawi.

‘Mwana wa uharibifu’ wa nyakati za mwisho ni mnyama aliye na pembe kumi wa Ufunuo 13 na Mfalme wa Kaskazini wa Danieli 11.

#### **Masalio ya Wafildefia ya Nyakati za Mwisheso Wasikose Kumtambua Mtu wa Kuasi**

Kuelewa utambulisho wa mtu wa kuasi katika 2 Wathesalonike 2 siyo tu suala la masomo ya mafundisho ya kidini kama vile wengine wanaamini. Hakika, kama unabii mwininge usio wa kibiblia ni ukweli, Masalio ya Wafildefia wa Kanisa la Mungu hawapaswi kutotambua ‘mtu wa kuasi’

kama vile Makanisa mengine ya Mungu wamekosa kumjua.

Kumbuka tena kitu katika 2 Wathesalonike 2:

9 yule ambaye kuja kwake ni kwa mfano wa kutenda kwake Shetani, kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo;10 na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa.11 Kwa hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu, waumini uongo;12 ili wahukumiwe wote ambaeo hawakuiamini kweli; bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu. (2 Wathesalonike 2:9-12)

Kuna ‘unabii wa kisiri’ wa Warumi na Othodoksi wa Mashariki ambaeo unasema kuwa kiongozi wao, ambaye mara nyingi huitwa ‘Mtawala Mkuu’ atakuja na ishara na zitathibitishwa na miujiza.

Tazama mmoja kutoka kwa Othodoksi wa Mashariki:

*Kinukuu bila majina* (Karne ya 10):Mfalme mmoja wa ukweli...anatarajiwa kujitokeza (kufunuliwa)...kwa njia za...ishara...Mfalme atasikia sauti na maagizo ya Malaika ambaye atamtokezea ana maono na anaelewa muktadha wa unabii...jina la Mfalme huyu Mfalme limefichwa (Limefichika) mionganii mwa mataifa...na jinsi mfalme huyu atakavyojitokeza kwa umma [ulimwengu] itafanyika kwa njia ifuatayo:Nyota itajitokeza [itaonekana] kwa siku tatu mfululizo na katika saa ya tatu ya usiku,na usiku na siku kuu ya Mama wa Aliye Juu (itakuja kuonekana) katikati ya Mji.Na hii nyota si mionganii mwa sayari...na mjumbe anayeongea kwa sauti kubwa katika siku tatu atawaita na kufunulia

wanaotumaini kwa umoja..Itakuja kuonekana katika mawingu “anga yasiyokuwa na ufasili ya jua”...chini ya mfano huo itaonekana msalaba inayoning’inia...Na mjumbe asyeonekana kutoka mbinguni na sauti yake kama ya radi atamwambia watu:Je huyu mtu mnakubali? Kwa wakati huo kila mtu atachukuwa na hofu na tishio...watampandisha juu kwa haraka na kumtangaza kama Mtawala wao Aliyerithi (Tzima Otto, H. The Great Monarch and WWIII in Orthodox, Roman Catholic, and Scriptural Prophecies. Verenika Press, Rock City (SC),2000, PP. 30,31,32,50-51,52,53).

Maonyesho ya msalaba yanayohusiana na Mtawala Mkuu (anayeitwa ‘Mfalme mmoja wa kweli’ hapo juu), ikifanyika, atadanganya watu kwa kufuata Mnyama-Biblia inaonya kwamba ulimwengu wote utamsujudu Mnyama huyu (Ufunuo 13:4,8) na wengi hawajagundua kwamba msalaba inaweza kutumika na Shetani.

‘Ndugu’ Mkatoliki alidai kujifundisha yafuatayo kutoka kwa ‘Maria’:

Kabla ya dhiki kuu, kutakuwako na ishara. Tutaona katika anga **msalaba mmoja mkubwa na mwekundu** katika mchana wa anga ya bluu bila mawingu...msalaba hii itaonekana na kila mtu: Wakristo, wapagani, wakafiri, nk, na pia na wenyewe wamekuwa tayari...ambao wataongozwa katika njia ya Kristo.Watapokea neema ya kupambanua umuhimu wa msalaba. (Flynn T, Flynn M. The Thunder of Justice.Maxkol Communications, Inc.Sterling (VA),1993, p.349)

Kwa hivyo, kukuja huku ambako kumenenwa hapo juu kupitia kwa inayokusudiwa kama masuka ya Maria inasema kwamba watu wataongozwa

kuelewa kuhusu msalaba katika anga. Lakini kwa vile Biblia haitabiri tukio hili kama kitu chema, hii ikitukia, inafaa ijulikane kwamba imetoka kwa Shetani.Msalaba hazikuwa ishara za Wakristo wa awali. Msalaba zilikubaliwa kwa upana na Wagiriki-Rumi amba walidai kuwa Wakristo baada ya Mtawala wa Rumi Konstantino na mamaye Helena aliziedeleza msalaba katika karne ya 4.

Kumbuka kwamba kulingana na ‘unabii’ watu wataombea ‘moyo safi wa Maria’ (mambo mengi kuhusu Maria yako katika makala Mary, the Mother of Jesus and the Apparitions/Maria, Mama wa Yesu na Masuka) na Mfalme (the Biblical King of the North/Mfalme wa Kaskazini wa Biblia) atachipuka.’Maria’ na ‘Mtawala Mkuu’ watapewa sifa kwa kuleta ‘amanii.’ Biblia pia inaonya:

3 Wakati wasemapo, Kuna amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafula, kama vile utungu umjiavyo mwenye mimba, wala hakika hawataokolewa. (1 Wathesalonike 5:3)

Watu watadanganya na madai, ishara na ajabu za uongo na zingine zitaonekana katika anga.

Kwa sababu Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) wanajua vizuri utambulisho wa mtu wa kuasi, itakuwa rahisi kwetu kuwaelezea wale watakaopenda kusikia kwamba ikiwa ‘msalaba’ ni ishara ambayo inatambua Mtawala Mkuu, basi hiyo hamwonyeshi mtu atakayechaguliwa Mungu, badala yake ni mtu aliyechaguliwa na Shetani. (tazama pia makala katika [www.cogwriter.com](http://www.cogwriter.com) inayo mada ya Satan’s Plan).

#### Amini Kinachofundishwa na Biblia

Wale ambaeo hawajui huyu ‘mtu wa kuasi’ hawatagundua kwamba unabii mwingine wa siku za mwisho unatimilika wakati unabii unatimilika. Kwa sababu hawatatambua, hawataweza kuwaonya

watu wao vizuri hata na ulimwengu kuhusu yanayofanyika. Wale ambao hawajui utambulisho wa mtu wa kuasi wanaweza kosa kulindwa kutoka kwa wakati wa majaribio uwajiao ulimwengu wote.

Yesu aliahidi kuwalinda Wafiladelfia wa Kweli kutoka kwa majaribio (Ufunuo 3:7-10) na sio tu wanaojiita Filadelfia (Ufunuo 3:9). Wengi katika makundi ya makanisa ya Mungu hawajui utambulisho kamili wa mtu wa kuasi. Kwa vile Wakristo wengi katika nyakati za mwisho sio sehemu ya masilio ya Wafiladelfia ya Kanisa la Mungu, hawatalindwa-lakini watapata wamekuwa chini ya ghadhabu ya shetani kulingana na Ufunuo 12:17.

Wengi wanategemea mapokeo yasiyofaa badala ya yale yaliyofundisha katika Biblia.

Yesu alikemea viongozi wa dini ambao walitegemea mapokeo kuliko neno la Mungu:

8 Ninyi mwaiaacha amri ya Mungu,  
na kuyashika mapokeo ya  
wanadamu. 9 Akawaambia, Vema!  
Mwaikataa amri ya Mungu mpate  
kuyashika mapokeo yenu. (Marko  
7:8-9)

Kwa hivyo, kwa muhtasari, neno la Mungu linafundisha nini kuhusu utambulisho wa mtu wa kuasi? Agano Jipyä linafundisha kwamba mtu wa kuasi " ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa" (2 Wathesalonike 2:4).

Agano la Kale linafundisha kwamba Mfalme wa Kaskazini "atajituza na kujihadhimisha juu ya kila mungu" (Danieli 11:36).

Agano Jipyä linafundisha kwamba "wote wakao juu ya nchi watamsujudu" (Ufunuo 13:8), Mnyama wa kwanza, mnyama aliye na pembe kumi (Ufunuo 13:1).

Ibada hii hailekezwi kwa nabii ya uongo. Na Biblia inafundisha kwamba nabii wa uongo, mnyama wa pili wa Ufunuo 13

"aifanya dunia na wote wakao ndani kumsujudu mnyama wa kwanza" (Ufunuo 13:12).

Soma peke yako katika Biblia yako.

Hata kama watamsujudu wanyama hao wote, maelezo katika Biblia ambayo yanaeleza mnyama aliye na pembe kumi/ Mfalme wa Kaskazini yako karibu sana na mtu wa kuasi ambaye ameelezwa katika 2 Wathesalonike 2:3-4 kuliko maelezo yo yote kuhusu nabii wa uongo.

Wale wanaolewa vizuri unabii na wanaosoma neno la Mungu wakiomba wapate mafundisho wanapaswa kugundua hii.

## Mtu wa Kuasi na Amri Kumi



### Maelezo ya Amri Kumi katika Hibrania

Na Bob Thiel

Wanafunzi wa Yesu walimwuliza yatakayotukia nyakati za mwisho (Mathayo 24:3). Hapa ni baadhi ya yaliyosemwa na Yesu kwamba tutaona:

12 Na kwa sababu ya kuongezeka kwa maasi, upendo wa wengi utapoa.13 Lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka. (Mathayo 24:12-13)

Maasi yataongezeka na upendo duni. Heshima duni kwa amri ya Mungu.Lakini bado, waaminifu wachache watakaodumu mpaka mwisho wataokolewa.

4 Kila atendaye dhambi, afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi. (1 Yohana 3:4 KJV)

4 Kila atendaye dhambi, afanya maovu pia, na maovu ni dhambi. (1 Yohana 3:4, DRB).

Mtume pia aliandika:

3 Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yo yote; maana haiji, usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu;4 yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana

kwamba yeye ndiye Mungu.5 Je! Hamkumbuki ya kuwa wakati nilipokuwapo pamoja nanyi naliwaambieni hayo? 6 Na sasa lizuialo mwalijua, yule apate kufunuliwa wakati wake.7 Maana ile siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi; lakini yupo azuiaye sasa, hata atakapoondolewa. (2 Wathesalonike 2:3-7)

Mtu wa kuasi anaimarisha dhambi. Anahuishwa na "siri ya uasi" ambayo pia inaitwa 'siri ya uovu' kwa sababu ataacha kuwa mtu wa dini na mtu wa nidhamu. Watu ambao hawajakubali imani ya ukweli, watamfuata.

Biblia inaonyesha kwamba mtu huyu wa kuasi, mamlaka ya Mnyama atakiuka amri zote kumi.

Wacha tuangalie kila amri Kumi.

Kwa amri ya kwanza, kumbuka ifuatayo kuhusu mtu wa kuasi, anayeitwa 'mfalme':

36Naye mfalme atafanya kama apendavyo; naye atajitukuza na kujiadhimisha juu ya kila mungu, naye atanena maneno ya ajabu juu ya Mungu wa miungu, naye atafanikiwa mpaka ghadhabu itakapotimia; maana yaliyokusudiwa yatafanyika.37 Wala hatajali miungu ya baba zake; wala yeye aliyetamaniwa na wanawake; wala hatamjali mungu awaye yote; maana atajitukuza mwenyewe juu ya wote. (Danieli 11:36-37)

Mfalme huyu ni Mfalme wa Kaskazini, ambaye anaitwa Mnyama "wa bahari" katika Ufunuo 13:1 na "mnyama wa kwanza" katika Ufunuo 13:12.

Mpinga Kristo ndiye "mnyama" wa pili na ndiye mnyama wa "nchi" (Ufunuo 13:11). Mpinga Kristo wa mwisho ataunga mkono mnyama wa kwanza na atajaribu

kuwalazimisha watu dhidi ya kutunza amri ya kwanza:

12 Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona. (Ufunuo 13:12)

Kulingana na vile amri ya pili inavyoenda, tazama atakayofanya Mnyama:

38 Lakini katika mahali pake atamheshimu mungu wa ngome; na mungu ambaye baba zake hawakumjua atamheshimu, kwa dhahabu, na kwa fedha, na vito vyta thamani, na vitu vipendezavyo. (Danieli 11:38)

Mpinga Kristo atajaribu kulazimisha watu dhidi ya kutunza amri ya pili:

14 Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo mnyama, akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliye kuwa na jeraha la upanga naye akaishi. 15 Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe. (Ufunuo 13:14-15)

Kuabudu sanamu hakika ni alama ya mnyama (hata hivyo mamlaka ya Mnyama anaweza kuvitumia vifaa kama vile msalaba, ambavyo wengi watakubali).

Kuhusu amri ya tatu, tazama yafuatayo:

25 Naye atanena maneno kinyume na Aliye juu, (Danieli 7:25)

16 Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kiume, au katika

vipaji nya nyuso zao; 17 tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake. (Ufunuo 13:16-17)

...wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake na kila aipokeaye chapa ya jina lake. (Ufunuo 14:11)

Pengine Mnyama atarekebisha kalenda na kubadilisha siku za wiki. Wengi wamehis ikwamba kuadhimisha Jumapili ilikuwa ama ndiyo ‘alama ya mnyama.’

‘Alama ya mnyama’ inahu kuvunja amri kumi.

Kulingana na amri ya tano, ntazama yafuatayo:

37 Wala hataijali miungu ya baba zake (Danieli 11:37).

Hii inaonyesha hajaheshimu wazazi wake, ijapokuwa hiyo si wazi sana. Zaidi ya hayo, Mnyama atamsaliti kahaba wake ambaye ni mama yake wa kiroho-na hatatubu:

16 Na zile pembe kumi ulizoziona, na huyo mnyama, hao watamchukia yule kahaba, nao watamfanya kuwa mkiwa na uchi. watamla nyama yake, watamteketeza kabisa kwa moto. 17 Maana Mungu ametia miyoni mwao kufanya shauri lake, na kufanya shauri moja, na kumpa yule mnyama ufalme wao hata maneno ya Mungu yatimizwe. 18 Na yule mwanamke uliyemwona, ni mji ule mkubwa, wenye ufalme juu ya wafalme wa nchi. (Ufunuo 17:16-18)

Kulingana na vile amri ya sita inavyoenda, mnyama atauwa kama kiongozi wa kijeshi:

4 Wakamsujudu yule joka kwa sababu alimpa huyo mnyama uwezo wake; nao wakamsujudu yule

mnyama, wakisema, Ni nani afananaye na mnyama huyu? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye? (Ufunuo 13:4)

Mnyama atasababisha wengine pia wauawe:

15...hata ile sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe. (Ufunuo 13:15)

32 na wao wafanyao maovu juu ya lile agano atawapotosha kwa maneno ya kujipendekeza; lakini watu wamjua Mungu wao watakuwa hodari, na kutenda mambo makuu.33 Na hao walio wenyewe hekima katika watu watafundisha wengi; hata hivyo wataanguka kwa upanga, na kwa moto, na kwa kufungwa, na kwa kutekwa nyara, siku nyingi. (Danieli 11:32-33)

Kama vile amri ya saba inavyoenda, mnyama atakuwa mionganoni mwa wale ambao watafanya usinzi na Babeli Mkuu:

1...Njoo huku nitakuonyesha hukumu ya yule kahaba mkuu aketiye juu ya maji mengi 2 ambaye wafalme wa nchi wamezini naye, nao wakao katika nchi wamelevya kwa mvinyo ya uasherati wake.3 Akanichukua katika Roho hata jangwani,nikaona mwanamke,ameketi juu ya mnyama mwekundu sana,mwenye kujaa majina ya makufuru,mwenye vichwa saba na pembe kumi.4 Na mwanamke yule alikuwa amevikwa nguo ya rangi ya zambarau,na nyekundu ,amepambwa kwa dhahabu,na kito cha thamani,na lulu,naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake,kilicho jawa na machukizo,na machafu ya uasherati wake.5 Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina

limeandikwa,la siri,BABELI MKUU  
MAMA WA MAKAHABA NA  
MACHUKIZO YA NCHI.(Ufunuo 17:1-5)

Mnyama atashiriki na kuimarisha usinzi wa kiroho (Yakobo 4:4; Ezekiel 23:37).

Kama vile amri ya nane inavyoenda, mnyama atachukua nchi zingine na kuchukua vitu vyao:

39 Naye ataziteka nyara ngome zenye nguvu kwa msaada wa mungu mgeni; na ye ye atakayemkubali atamwongeza kwa utukufu; naye atawapa kumiliki wengi; naye ataigawa nchi kwa rushwa,40 na wakati wa mwisho mfalme wa kusini atashindana naye; na mfalme wa Kaskazini atamshambulia kama upepo wa kisulisuli, pamoja na magari ya vita, na wapanda farasi, na merikebu nyingi; naye ataingia katika nchi hizo, na kufurika na kupita katikakati. ...43 Lakini atakuwa na nguvu juu ya hazina za dhahabu na fedha, na juu ya vitu vyote vya Misri vyenye thamani, na Walibia na Wakushi watafuata nyayo zake. (Danieli 11:39-40,43)

Mnyama atachukua nchi na vitu vya thamani.

Kam vite amri ya tisa inavyoenda, mnyama atasababisha uongo kustawi:

25 Atasababisha udanganyifu ustawi. (Danieli 8:25)

23 Baada ya kufanya mapatano naye, atatenda kwa udanganyifu, pamoja na watu wachache tu ataingia madarakani. (Danieli 11:23)

Watu ambao hawana "upendo wa ukweli" wataamini uongo (2 Wathesalonike 2:12). Uwongo unaohimizwa na 'miujiza' (2 Wathesalonike 2:8-11; Ufunuo 13:11-15), ulaghai wa kiuchumi (Ufunuo 13:16-18), na

meteso (Danieli 11:31-35; Ufunuo 13:7). Kama vile amri ya kumi inavyoenda, kumbuka yafuatayo:

25...naye atasimama kushindana na aliye Mkuu wa wakuu; lakini atavunjika, bila kazi ya mikono. (Danieli 8:25)

24 Naye atachochea nguvu wake na ushujaa wake juu ya huyo mfalme wa kusini kwa jeshi kubwa; na mfalme wa kusini atafanya vita kwa jeshi kubwa mno lenye nguvu nyingi; lakini hatasimama; maana watunga hila juu yake. (Danieli 8:24)

Mnyama ana tamaa ya nguvu na milki na atabuni mipango ya kuchukua visivyo vyake. Anataka hata nguvu za Mungu.

Mnyama atakiuka amri zote kumi za Mungu na kutarajia wafuasi wake kufanya hivyo.

Maandiko yanaonyesha kwamba kukiuka kila Amri Kumi ni kutenda dhambi.k.v. ya kwanza 1 Samueli 15:24-25; ya pili Kutoka 32:22-30; ya tatu Ayubu 2:9-10 (Zaburi 39:1); ya nne Nehemia 9:14,28-29; ya tano Luka 15:18 (1 Samueli 24:11);ya sita Mwanzo 4:7;ya saba Mwanzo 39:9;ya nane Mathayo 5:30 (Mwanzo 31:30,36); ya tisa Kumbukumbu 23:21;ya kumi Warumi 7:17.

Kumbuka kwamba Biblia inaita huyu mvunjaji amri “mtu wa kuasi...mwana wa uharibifu, ambaye anapinga na kujitokuza juu ya kila aitwaye Mungu ama anayeabudiwa” (2 Wathesalonike 2:3-4).

### Nyakati za Hatari

Mtume Paulo alitiwa msukumo kuandika yafuatayo kuhusu nyakati za mwisho:

1 Lakini ufahamu neno hili ya kuwa siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari.2 Maana watu watakuwa wenyewe kujipenda wenye,wenye kupenda fedha,,wenye kujisifu,wenye kiburi,wenye kutukana,wasiotii wazazi

wao,wasio na shukrani,wasio safi,3 wasiowapenda wa kwao,wasiotaka kufanya suluhu,wasingiziaji,wasiojizuia,wakali,wasiopenda mema,4 wasaliti,wakaidi,wenye kujivuna,wapenda anasa kuliko kumpenda Mungu;5 wenyewe mfano wa utauwa lakini wakikana nguvu zake;hao nao ujiepushe nao.6 Kwa maana katika hao wamo wale wajiingizao katika nyumba za watu,na kuchukua mateka wanawake wajinga wenyewe mizigo ya dhambi,waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi;7 wakijifunza siku zote,ila wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kweli.(2 Timotheo 3:1-7)

Wakati yaliyo juu yanajumuisha wengi, hata wanasiasa, tazama jinsi haya yanaeleza juu ya Mnyama.

- Wenyewe kujipenda wenye: Mnyama atafanya hivyo (Danieli 11:36). Hii ni kuweka tofauti kati ya kumpenda Mungu na jirani, hivyo atakiuka Amri zote Kumi.
- Wenyewe kupenda fedha: Mnyama ataiba “hazina ya dhahabu na fedha, na... vitu vyote vya Misri vyenye thamani” (Danieli 11:43) na mengine mengi.
- Wenyewe kujisifu: Mnyama atajivuna katika kiburi chake (Danieli 7:25; Yakobo 4:16) katika kukiuka amri ya tisa.
- Wenyewe majivuno: kuvunja amri ya tisa itakuwa nembo ya Mnyama (Danieli 11:36).
- Wenyewe kumkufuru Mungu: Biblia inasema kwamba Mnyama “atanena maneno ya kumkufuru Mungu wa miungu” (Danieli 11:36; Ufunuo 13:6) katika hali ya kukiuka amri ya tatu.

- Wasiotii wazazi: Hii pia inadokezwa kwa Mnyama katika Danieli 11:37.
- Wasio na shukrani: Mnyama hatakuwa na shukrani kwa Mungu wa kweli (Danieli 11:36).
- Wasio safi: Sheria na Amri ni takatifu (Warumi 7:12), lakini Mnyama atawatukuza wale wanaokiuka agano takatifu (Danieli 11:37).
- Wasiowapenda wa kwao: Mnyama ni mwabudu sanamu, mwuaji, na mtesaji (Ufunuo 13) ambaye amekosa baadhi ya asili ya huba, upendo (Danieli 11:37).
- Wasiopenda kupatanishwa: Biblia haipendekezi kwamba Mnyama atakuwa na msamaha (Danieli 11:40; Ufunuo 13:10).
- Wasingiziaji: Mnyama atakufuru, na kutoa maelezo ya kikatili ya masingizio (Ufunuo 13:5-6;2 Wathesalonike 2:10), na kudanganya (Danieli 11:27) katika kukiuka amri ya tatu na ya tisa.
- Wasiozuia tamaa zao: Mnyama atakasirika (Danieli 11:30), na kujitokuza zaidi (Danieli 11:30-32).
- Wakatili: Mnyama atawatesa watakatifu (Danieli 7:25; Ufunuo 13:7).
- Wasiopenda mema: Mnyama atakula njama dhidi ya watu wa agano takatifu (Danieli 11:30-32).
- Wasaliti: Mnyama atahamasisha usaliti (Danieli 11:30-32) kwa kukiuka amri ya tatu na ya kumi.
- Wakaidi: Mnyama atakuwa mkaidi (Danieli 11:29-43).
- Waliojaa majivuno: Mnyama atajivuna (Danieli 11:36-37; Ufunuo 13:5-8).
- Wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu: Mnyama anajipenda sana na anapenda anachotaka kuliko Mungu (Danieli 11:36-37) kwa kukiuka amri ya kwanza.
- Wenye mfano wa utauwa: Mnyama atadai kuwa na dini (Danieli 11:38) na atafanya kazi na nabii wa uongo (Ufunuo 16:13-14). Lakini dini hiyo itakuwa ya uongo na wabuudu sanamu (Ufunuo 13:14-15).
- Wakizikana nguvu za Mungu: Mnyama atazikana nguvu za Mungu na kuwa mwasi (2 Wathesalonike 2:8-10).
- Kuchukua mateka wajinga wenye mizigo ya dhambi na tamaa: Mnyama atazajiri ‘miujiza’ (2 Wathesalonike 2:8-11; Ufunuo 13:11-15), ulaghai wa kiuchumi (Ufunuo 13:16-18), ‘kufurahi katika udhalimu’ (2 Wathesalonike 2:12), na kutesa (Danieli 11:31-35; Ufunuo 13:7) ili awafanye watu kumwabudu na kupokea chapa yake. Amri zote za Mungu ni ya haki (Zaburi 119:172).
- Hawawezi Kuufikia ujuzi wa Ukweli: Mnyama ataudai uongo mwangi kama ukweli, na kwa huzuni wengi wataenda pamoja na uongo huo kwa sababu hawakupokea upendo wa ukweli ili watunze amri (2 Wathesalonike 2:7-12).

Paulo anaonya dhidi ya watu katika nyakati za mwisho ambao hawazingatii amri za Mungu.Na hiyo inajumuisha mvunjaji wa amri ambaye ni ‘mtu wa kuasi.’

## Siku Kuu ya Baragumu



Na Bob Thiel

Makanisa mengi ya Wagiriki-Rumi hawaadhimishi siku kuu za kibiblia ambazo kwa kawaida zinafanya katika Majira ya kupukutika. Na bado Siku kuu hizi zinaonyesha matukio ya kimsingi katika mpango wa Mungu.

Siku Kuu ya Baragumu inaonyesha kurudi kwake Kristo kufufua malimbuko ya kwanza kutoka kwa wafu na pia inaonyesha nyakati za hatari ya maangamizo ambazo ziko mbele na kuingilia kati kwa Yesu Kristo kuokoa binadamu kutoka kwa uharibifu na kusimamisha Ufalme wa Mungu duniani.

Hili ni jambo kuhusu Siku Kuu hii kutoka kwa maandiko ya Kihibrania:

23 Kisha BWANA akanena na Musa, na kumwambia, 24 nena na wana wa Israeli, uwaambie, Mwezi wa saba, siku ya kwanza ya mwezi, kutakuwa na kustarehe kabisa kwenu, ni ukumbusho wa kuzipiga baragumu, ni kusanyiko takatifu. 25 Msifanye kazi yo yote ya utumishi; (Walawi 23:23-25)

Wacha tuelewe jinsi siku kuu hii inafaa katika mpango mkuu wa Mungu.

Kumbuka kwamba kuna mwanya mkubwa sana kati ya Siku ya Pentekoste na Siku kuu ya Baragumu. Kwa vile Kanisa la Agano Jipya lilianza siku ya Pentekoste na inaisha wakati Yesu atakaporudi wakati wa baragumu ya mwisho (1 Wakorintho 15:51-57), kwa kawaida muda huo kati ya Pentekoste na Siku Kuu ya Baragumu unaweza kuzingatiwa kuwa unaonyesha

kipindi cha kanisa-kipindi ambacho tuko sasa!

Siku kuu ya nne, Siku kuu ya Bragumu, inaadhimishwa "mwezi wa saba, katika siku ya kwanza ya mwezi huo" (Walawi 23:23-25).

Nambari saba katika mpango wa Mungu inaashiria ukamilifu na utimilifu. Mwezi wa saba katika kalenda ya Mungu (ambao unapatikana katika Septemba na/ama Oktoba) una Siku kuu nne za mwisho, ambazo zinaashiria ukamilifu wa mpango mkuu wa Mungu kwetu sisi. Siku kuu ambayo inapatikana katika siku ya kwanza ya mwezi huu inaonyesha mwanzo wa matukio ya mwisho katika mpango wa Mungu.

Vile kitabu cha Walawi imeonyesha, ni Sabato nydingine ya mwaka ya kupumzika kwa kazi za kawaida, ni makumbusho ya kupiga baragamu. Pia ni wakati wa kufundisha njia za Mungu (Nehemia 8:2-3; Ezra 3:1-7). Mengi yaliyoandikiwa wana wa Israeli yaliandikwa kuwa kielelezo kwetu "kwa jinsi ya mifano yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani" (1 Wakorintho 10:11). Ni kwa sababu ya kupiga baragumu ndiyo maana Siku kuu hii inaitwa Siku kuu ya Baragumu.

Kuna maana kuu ya ishara ihusianayo na kupiga baragumu, haswa na nyakati za hatari tunamoishi. Inafaa ikumbukwe kwamba jina la kiyahudi ya tarehe hii, Rosh Hashanah, silo la kibiblia na hata si ya awali kwa Wayahudi. Ni kitu walipata karne nydingi baada ya Mungu kuwapa Siku kuu na baada ya kuandikwa kwa Agano la Kale (Kramer,Amy J.Rosh Hashana Origins,Copyright©1998-1999Everything Jewish,Inc.).

Biblia inafundisha kwamba baragumu zilikuwa zinapigwa kutangaza Siku kuu za Mungu, na pia kuwaita watu wasanyike (Hesabu 10:1-3,10).

## **Kitabu cha Uzima**

Ya ajabu ni kwamba wasomi Wayahudi wamelinganisha Sikuu ya Baragumu na ‘Kitabu cha Uzima’ (Peltz M, Rabbi. What is in a Rosh Hashanah greetings? Haaretz, September 17, 2012). Kwa nini ni kitu cha ajabu?

Biblia inafundisha kwamba wale walioorodheshwa katika ‘Kitabu cha Uzima’ (Wafilipi 4:3; Ufunuo 3:5) watafufuliwa (Waebriana 12:22-23). Lini? Wakati wa Bragumu ya saba ambayo ni ya mwisho:

51 Angalieni, nawaambia ninyi siri; hatutalala sisi sote, lakini sote tutabadilika, 52 kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na watu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika. 53 Basi huu uharibikao utakapovaa kutokuharibika, na huu wa kufa utakapovaa kutokufa. (1 Wakorintho 15:51-53)

Kitabu cha Ufunuo kinafundisha vizuri kwamba baragumu saba zitapigwa (8:2), na mapigo yanakuja kwa wale wasiolindwa na Mungu (9:4), na Ufalme wa Mungu na hukumu utakuja (11:15-18). Ya mwisho inafundisha kwamba wale amba majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima watakuwa kifo cha pili (Ufunuo 20:14-15).

## **Milio ya Baragumu**

Kumbuka kwamba Biblia inaonyesha kwamba wakati wa historia ya Israeli, ambao uliakifishwa na migogoro na uasi, baragumu zilitumika kama vifaa vya kuonya, kuwaita wanajeshi ama kama utangulizi wa mambo muhimu-mara nyingi kuashiria matukio makuu ya kuagiza taifa zima.

Mungu pia alitumia manabii, miongoni mwao Isaya, Ezekiel, Hosea na Yoeli

kuwaonya Waisraeli kuhusu ghadhabu angeleta kwao kwa kuzidi kuasi dhidi ya sheria za Mungu. Hawa manabii wangetumia sauti zao kama baragumu kuyalipua maonyo yao kwa watu wa Mungu.

1 Piga kelele, usiache, Paza sauti yako kama tarumbeta; Uwahubiri watu wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao. (Isaya 58:1)

Sisi tulio katika Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) tunafanya hivyo leo. Tunawaambia jamii dhambi zao kwa wazi na jinsi matukio ya ulimwengu yanapangana sawasawa na unabii unaoleweka-ambao tunajaribu kufanua.

Lakini kutakuwako na milio ya baragumu ambayo inakuja nyakati zijazo kama vile kitabu cha Ufunuo kinavyofundisha (Ufunuo 8:1-13, 9:1-18). Lakini wengi hawatajihadhari maonyo hayo.

Nyingi zimepigwa katika Kitabu cha Ufunuo, na nyingi zingepigwa katika Siku kuu ya Baragumu (Walawi 23:24)-kwa matumaini wengi wameanza kuuona uhusiano huu.

Lakini baragumu muhimu sana, kwa kawaida, ni ya mwisho, ile ya saba. Ufunuo inafundisha hivi kuhusu hiyo:

15 Malaika wa saba akapiga baragumu, pakawa na sauti kuu katika mbingu, zikisema, Ufalme wa dunia umekwisha kuwa Ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atamiliki hata milele na milele. 16 Na wale wazee ishirini na wanne waketio mbele za Mungu katika viti vya enzi vyao wakaanguka kifulifuli, wakamsujudia Mungu 17 wakisema, Tunakushukuru wewe, Bwana Mungu Mwenyezi, uliyeko na uliyekuwako, kwa sababu umeutwaa uweza wako ulio mkuu, na kumiliki. 18 Na mataifa walikasirika, hasira

yako nayo ikaja,na wakati ukaja wa kuhukumiwa waliokufa,na wa kuwapa thawabu yao watumwa wako manabii na watakatifu,na hao walichao jina lako,wadogo kwa wakubwa,na wa kuwaharibu hao waiharibuo nchi.19 Kisha Hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa,na sanduku la agano lake likaonekana ndani ya hekalu lake.Kukawa na umeme,na sauti,na radi,na tetemeko la nchi,na mvua ya mawe nyangi sana.(Ufunuo 11:15-19)

Siku kuu ya Baragumu inaonyesha kupigwa kwa baragumu nyakati zijazo na hakika kwamba Yesu atarudi na kuanzisha Ufalme wa Mungu duniani. Habari njema ya Ufalme wa Mungu ni sehemu kubwa ya injili Yesu anataka watumishi wake waitangaze (Mathayo 24:14). Siku kuu ya Baragumu inaonyesha ushindi wa Kristo juu ya ulimwengu.

Wanahistoria wa Wagiriki-Rumi, kama vile Jerome na Epifaniasi (Catholica Omnia Tabulinum De Ecclesiae Patribus Doctoribusque Materia Migne JP Argumentum Patrologia latina Volumen MPLO25 Ab ColumnaadCulunnam 1415-1542A.pp.922,930), walirekodi kwamba ‘Wakristo Wanazareti’ waliendelea kuadhimisha Siku kuu ya majira ya kupukutika katika karne ya nne mpaka waliposimamishwa na mamlaka ya kifalme (see pixner B. Church of the Apostles Found on Mt. Zion. Biblical Archeology Review, May/June 1990:16-35,60).

Wapinga-Semiti John Chrysostom hasa alijaribu kukataza watu wasiadhimishe Siku kuu ya Baragumu katika mwisho wa karne ya nne (John Chrysostom.Homily 1 against the Jews 1:5; VI:5; VII:2. Preached at Antioch, Syria in the Fall of 387 AD, Medieval Sourcebook: Saint John Chrysostom (c.347-407).

Hata hivyo, waliokuwa waaminifu walijaribu kuadhimisha siku hiyo siku zote katika historia.

Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) wanafanya hivyo hadi sasa.

## Je Mungu Anakuita?



1896 Simu kutoka Uswidi

Na Alfred E. Carrozzo (*awali ilichapishwa katika Jarida la ulimwengu wa Kesho, Mei 1971; na maandiko mapana yaliyohaririwa bado na Bob Thiel*)

Katika dakika hii Mungu anawaita watu watoke katika ulimwengu huu uliolemewa na ugonjwa wa dhambi na unaokaribia kufa. Ni wito wa ajabu kwa kusudi la kipekee. Ni msukumo-khofu kwamba wengine wana ugumu wa kuamini. Pengine unaitwa sasa hivi. Unafaa ujue, usije ukapuuzia wito mkuu kutoka kwa Mungu mkuu wa ulimwengu wote. Soma makala hii na uchunguze kama Mungu anakuita!!

Dhana ya KAWAIDA ya Wakristo wa ulimwengu wa leo ni ya kwamba kuna mapambano dhidi ya Mungu na Shetani. Dhana hii inafundisha kwamba Mungu anajaribu kuokoa kila mtu, na Shetani anajaribu kupoteza watu wote. Ikiwa hiyo ni ukweli, basi mtu ye yote mwaminifu atakubali kwamba MUNGU ANASHINDWA!

Watu wengi hapa duniani leo hii hata hawakiri Ukristo. Na bado, Biblia yako inasema hakuna jina jingine chini ya mbingu ambalo litupasalo kuokolewa kwalo (Matendo 4:12 "Wala hakuna wokovu katika mwininge awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.") Mamilioni ya watu wameishi na kufariki bila kusikia jina la Yesu Kristo. Je watu hawa watakuaje? Je mtoto ambaye aliishi masaa machache atakuwaje? Je Mungu amewaacha waadhibiwe? Na je watakuwaje mamilioni

ya watu walioishi katika jamii ya ukonaji Mungu? Je wamepotea milele?

SIYO HIVYO KABISA! KILA MTU atapata nafasi!

### Wito Maalum Ni Muhimu

Ukweli unaoshangaza ni kwamba Mungu hajaribu kuokoa kila mtu sasa! Ni ukosefu wa kuelewa mpango wa Mungu ndiko kunasababisha wainjiliisti wapige kelele: "Mpe Bwana moyo wako kabla hujachelewa sana!" Neno la Mungu liliotiwa msukumo linafunua kwamba HAKUNA ye yote anayeweza kuja kwa Yesu Kristo ISIPOKUWA BABA MWENYEWE AMEMWITA (Yohana 6:44 "Hakuna mtu auezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka; nami nitamfufua siku ya mwisho).

Kwa maneno mengine, leo hii SIYO SIKU PEKEE YA WOKOVU!! Huu ndio ukweli wa kutosha wa Biblia yako.

Wote ambaao hawajaitwa sasa, ama hawajapewa nafasi ya wokovu, watafufuliwa katika ufufuo wa pili. Watafufuliwa kama binadamu wa kawaida na kupewa nafasi moja na ya kipekee ya wokovu. Huu ufufuo unafanyika baada ya miaka elfu, baada ya kinachoitwa na wanafunzi wa Biblia "Milenia."

Wengi wanaokiri kuwa ni Wakristo hawajui ukweli huu. Kwa nini kuna kutojua katika kipindi hiki cha mwanga? Kwa nini watu ambaao wanajiita "Wakristo" hawaelewi maelezo rahisi ya wanayemda kuwa wanamfuata? Yesu Kristo mwenyewe aliwambia wanafunzi wake: "...Ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni, bali wao hawakujaliwa" (Mathayo 13:11). Aliwaelezea wafuasi walio wandani wake kwamba wao wameitwa. Alisema: "...mimi niliwichagua kutoka ulimwengu" (Yohana 15:19).

Biblia imejaa na THIBITISHO kwamba Wakristo wote lazima wapate wito kutoka kwa Mungu.

### Kuelewa Kumefunikwa

Hata kama inonekana ya kushangaza, Mungu alifunika na kuficha maana ya ujumbe wake kimakusudi ili watu wengi wasielewe. Mungu anaeleza katika Isaya 28:10-13:

“ Kwa maana ni amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni, huku kidogo na huku kidogo.”...ili waende na kuanguka nyuma, na kuvunjwa, na kunaswa, na kuchukuliwa.”

Mungu aliandika Neno lake kimakusudi ili watu wasielewe. Alikusudia kwamba wale tu anayewaita na kuwachagua ndio watakaoelewa.

Je unaelewa Neno la Mungu? Je Mungu anakuita! Unajuaje?

### Jinsi Mungu Anaita na Kuchagua

Wengi hawaelewi jinsi Mungu anaita. Wengine wanafikiri Mungu anaita kwa kutumia sauti. Wengine wanafikiri inafanywa kwa njia ya kuingia kati kwa maporomoko kama vile ajali au moto. Na bado wengine wanatamani “hisia nzuri kila mahali” ili wahakikishe kwamba wameitwa.

Ukweli ni nini? Mungu anaitaje? Je umewahi kuitwa na kuchaguliwa na Mungu? Jibu ni rahisi kuelewa. Kwa njia rahisi iliyotajwa, Mungu anaita kupitia kwa Injili yake na kupitia kwa Roho Mtakatifu.

Injili ni habari njema ya serikali ya Mungu inayokuja na imerekodiwa katika Biblia-Neno la Mungu kwa wanadamu. Kupitia Roho Mtakatifu wa Mungu, Mungu anafungua wale anaowaita ili waelewe ukweli wazi wa ujumbe wa Injili yake. Roho wa Mungu anaanza kufanya kazi katika njia ya kipekee na wale anaowaita.

### Atakayofanya Roho Mtakatifu

Ni jinsi gani Roho Mtakatifu ataonekana ndani ya wale wanaoitwa na Mungu? Ni jinsi gani Roho wa Mungu anafanya kazi kwa mwanadamu au kupitia kwa mwanadamu?

Kwanza kabisa, Roho wa Mungu ataongoza anayeitwa kuamini kwamba Mungu yupo! Katika nyakati hizi za ukonaji na shaka, ni kawaida kukataa kuwepo kwake Mungu. Lakini Roho wa Mungu anapofanya kazi na wewe, si rahisi kukataa uwepo wa Mungu. Ni ishara kwamba Mungu anakuita!

Pia, Roho wa Mungu atakuongoza kuthibitisha na kuamini Biblia kama Neno la Mungu lenye msukumo-Kitabu cha Mungu cha maagizo. Roho wa Mungu atakuongoza kujua, “16 Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki.” (2 Timotheo 3:16)

Ni jinsi gani mtu ye yote ataamini Biblia ikiwa anahisi kwamba sehemu zingine hazijatiwa msukumo? Na bado, hii ndiyo “Wakristo” wengi, vile wanavyoitwa, wameamini leo! Wengi wanazingatia Agano la Kale kama fasihi ya historia. Wengine wanaenda hatua kwa kufundisha kwamba kitabu cha Ufunuo ni maandiko ya mtu aliye na umajinuni wa njozi.

Wengine wanasema kwamba barua za Paulo ndizo zafaa kukubaliwa. NI UPUZI GANI HUO!

Kuchanganyikwa huku kwa maandiko ni matokeo ya kuchagua sehemu zingine za kuamini kwa Biblia-kukataa kukubali maandiko yote kama ilivyopewa na msukumo wa Mungu.

Inapaswa kuamini Biblia yote ama kutoamini kabisa. Ni rahisi hivyo. Yesu Kristo alisema:

“...maandiko hayawezi kutanguka” (Yohana 10:35).

Alisema maandiko yanafanya mfuatano ulio kamili-hayapingani. Na bado, vitabu vimeandikwa kufunua madai ya migongano. Lakini Yesu alisema maandiko hayatanguki.

Kila madai ya mgongano ni kwa mujibu wa utafsiri mbaya ama ufanuzi mbaya. Usipoendea maandiko na ukweli, huwezi kuelewa maana kamili ya Neno la Mungu. Utajidanganya kwa kuamini kwamba Biblia imejaa migongano na haiwezi kutegemewa.

Ikiwa umeamini Biblia ni Neno la Mungu-kwamba kila andiko limetiwa msukumo na Mungu-na kwamba maandiko hayawesi kutanguka,” Mungu huenda anakuita!

Njia nyingine ambayo Roho wa Mungu anaongoza wanaoitwa na Mungu ni kwa kuwatia msukumo ili wachukue Mungu kwa neno lake-kuamini kwamba amesema alichomaanisha na anamaanisha alichosema.

Wale wanaoitwa na Mungu kupitia Roho Mtakatifu wataamini maelezo rahisi yaliyorekodiwa katika Biblia bila kuyapaka na dhana nyingi ya kufikiriwa tu.

Ikiwa Mungu anakuita, Roho wake atakuongoza uamini Kristo hakuja kutangua Torati lakini kukamilisha na kuitekeleza (Mathayo 5:17 “Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la sikuja kutangua, bali kutimiliza.”). Utaamini Ufalme wa Mungu haupatikani mbinguni, bali ni hapa duniani. Utaamini maelezo yaliyo wazi kwamba wapole watairithi nchi-siyo mbinguni (Mathayo 5:3,5 “ 3 Heri walio maskini wa roho; Maana ufalme wa mbinguni ni wao, 5 Heri wenye upole; Maana hao watairithi nchi.).

Ikiwa Roho wa Mungu anafanya kazi kwako na anakuita, utakataa dhana ya kipagani ya roho isiyokufa. Utaamini maelezo katika Ezekiel 18:4,20, ( 4 Tazama,roho zote ni mali yangu,kama vile roho ya baba ni mali yangu;roho ile itendayo dhambi itakufa. 20 Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa;

mwana hatauchukua uovu wa baba yake, wala baba hatauchukua uovu wa mwanawe, haki yake mwenye haki itakuwa juu yake, na uovu wake mwenye uovu utakuwa juu yake.) Kwamba roho haiwezi kishi milele lakini inawezakufa!

Utaanza kuelewa kwamba yote uliyofundishwa kuhusu Biblia ni kinyume cha ukweli. Nafasi itaruhusu mifano michache hiyo, lakini kuna mambo mengi yasiyoleweka kuhusu alichosema Mungu ambayo yangeonyeshwa.

Ikiwa Roho wa Mungu anakuongoza, atakuongoza kuelewa Ukweli wazi wa Neno lake.

Zaidi ya hayo, Roho wa Mungu atakuonyesha kwamba USIJARIBU kutafsiri Biblia: “...hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu” (2 Petro 1:20).

Wengi hawawezi kuelewa maandiko kwa sababu hawajaelewa kuwa Biblia inajifasiri yenye! Migongano mingi inafanyika kwa sababu watu hawajafundishwa kuacha Biblia ijitafsiri. Kupitia kusoma kwa bidii na kwa makini, tunaweza kuelewa mistari inayokanganya kwa kupitia maandiko mengine.

Kwa mfano, Ufunuo 12:3 (3 Ikaonekana ishara nyingine mbinguni; na tazama joka kubwa jekundu, alikuwa na vichwa saba na pembe kumi, na juu ya vichwa vyake vilemba saba.) inataja “joka kubwa jekundu” aliye na vichwa saba na pembe kumi. Kumekuwako na tafsiri tofauti tofauti ya mstari huu. Wengine wanasema joka hili ni nabii wa uongo. Wengine wanasema ni mnyama. Na bado wengine wanadai joka ni ishara ya ajabu inayoonyesha Urusi Mwekundu ama aina ya Ukomunisti. Lakini tafsiri hizi zote siyo ya ukweli.

Mungu hajatuambia katika mstari wa tatu maana ya joka jekundu. Tukisoma mstari wa tatu peke yake tutasema kwamba hatujui maana yake. Ama tutakuja na

tafsiri yetu. Ama TUTAACHA BIBLIA IPATE KUJITAFSIRI YENYEWE!

Ikiwa tutaacha Biblia kujitafsiri, tunachohitajika KUJUA kinachomanishwa na joka jekundu ni kusoma mstari wa tisa. Katika mstari wa tisa Mungu anafafanua kwamba joka “nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani.”

Ikiwa Mungu anakuita, Roho wake atakuongoza kuamini kila maelezo ya Biblia, na utaacha Biblia itoe tafsiri yenyeve! Lakini hiyo bado haitoshi.

Roho wa Mungu ataongoza wale wanaoitwa naye KUISHI KWA KILA NENO LA MUNGU! (Mathayo 4:4.<sup>4</sup> Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.”) Ili uelewe Biblia, ni muhimu sana kuishi kwa kila neno la Mungu, siyo sehemu zingine ama mafundisho ya kubembeleza. Wengi wanaokiri kuwa Wakristo wanakubali ukweli mwingine wa Biblia, lakini kwa sehemu kubwa, wanatembea kwa njia hitilafu duni. Wanawezaji kuishi kwa Neno la Mungu wakati hawajui hata linalosema?

Ni uhakika wa kutisha kwamba wengi wanaokiri kuwa Wakristo hata hawawezi kutaja vitabu vya kwanza vya Agano Jipy-Vitabu vine vya Injili-Injili ambayo inafaa waamini!

Nikiongea kwa ukweli, karibia watu WOTE wanaokiri kuwa Wakristo HAWANA HAJA kuishi kwa kila neno la Mungu lakini wanachukua sehemu kidogo tu ambayo inahusu maisha yao. Mungu anawapa kuelewa kwa wale tu wanaotaka kuishi kwa kila neno lake!

Njia nyininge ambayo Mungu anatumia Roho wake kuwaita watu wake ni kwa kuwatia hatia na kuwashawishi kwa njia yake. Ikiwa Mungu anakuita, utaanza kuelewa kwa undani Biblia kwa mara ya kwanza. Utaanza kusoma na kujifunza Biblia na hamu ya jitu aliye aliyanbanwa na njaa. Na utakuja kugundua kwamba kuna

njia ioneukanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti (Mithali 14:12<sup>12</sup> Iko njia ioneukanayo kuwa sawa machoni pa mtu, Lakini mwisho wake ni njia za mauti.)

Njia ya binadamu ni kunya kua, ulafi, njia ya ubinafsi ya “kupokea.” Ni njia ya filosofia ya “kuwafanya wengine kabla hawajapata nafasi ya kukufanya”. Ni njia ya tama, husuda, ugomvi, uuaji, wivu, hasira, ulevi, nakadhalika. Ndiyo chanzo cha mateso, magonjwa ya moyo na masikitiko. Ndiyo sababu ya hali mbaya tunayoiona duniani leo.

Ikiwa Mungu anakuita, Roho yake atakushawishi uanze kukubali kwa ndani kwamba ulikuwa ukifanya vitu kwa njia ya binadamu, njia iongozayo kwa mauti. Utaanza kutoa maisha yako yote kwa Mungu na njia zake. Utasema, na kumaanisha, “mapenzi yako yatimizwe.” Utatubu!

Kupitia kwa kujifunza Biblia na kuwa karibu na Mungu, utaona vile ulimwengu mzima kwa hakika, “uko ukingoni mwa uharibifu kwa sababu ya njia za binadamu. Utakuja kujuwa kwamba binadamu yuko karibu kufika ukingoni mwake. Binadamu anahitaji usaidizi. Na Mungu ndiye anaweza kutupa majibu yote ya shida za ulimwengu.

Suluhihisho la shida za binadamu ni kufuata njia ya Mungu-njia ya uhusiano unaotoka nje-njia ya kutoa, kugawanya, kusaidia-njia ya kuwafanya wengine kama vile ungependa wakufanyie. Ni njia ya furaha kamili, fahari, amani, kutosheka-njia ya ungwana, wema, upole na kujithibiti. Imejengwa katika kanuni Kristo aliwapa wanafunzi wake kwamba kuna baraka kwa kutoa kuliko kupokea.

Ikiwa Mungu anakuita, anakutia hatia na kukushawishi kwa njia Yake, utaanza kuwa na amani ndani yako. Utaanza kuamini Mungu kwa kusuluhiha matatizo ya ulimwengu kupitia kwa njia Yake ya upendo. Utajua na kugundua kwamba

Mungu kwa ukweli ana majibu. Utafurahi katika uhakika kwamba Mungu ana majibu kwa wale wanaoitwa.

Na baadaye utaanza kufahamu kwamba Mungu anaita wengine sasa kwa kusudi fulani. Utagundua ni wito maalum kwa Kazi maalum. Ni tume la kipekee. Ni tume la kuhubiri Injili ya ukweli ya Ufalme wa Mungu ulimwenguni kote kama ushuhuda kabla ya mwisho wa dahari. Ni tume ya kufundisha mataifa yote kuamini kila kitu alichoamuru wanafunzi wake: Ni tume na Kazi iliobuniwa kuigeuza miyo ya kina baba kwa watoto wao, na miyo ya watoto kwa baba zao ili binadamu alindwe kwa kujiharibu mwenyewe! (Mathayo 24:14,21,22<sup>14</sup> Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja.<sup>21</sup> Kwa kuwa wakati huo kutakuwapo dhiki kubwa, ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala haitakuwapo kamwe.<sup>22</sup> Na kama siku hizo zisingalifupizwa, asingeokoka mtu ye yote; lakini kwa ajili ya wateule zitafupizwa siku hizo. Na Malaki 4:6<sup>6</sup> Naye ataigeuza miyo ya baba iwaelekee watoto wao, na miyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia laana.”)

Ikiwa Mungu anakuita, utaanza kufanya Kazi yake kwa moyo wako wote. Itagundua kwamba maarifa haya makubwa ya njia ya Mungu yanahitajika na ulimwengu wote. Utajua zaidi kwamba watu wa Mungu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa haya (Hosea 4:6<sup>6</sup> Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa, mimi naml nitakukataa wewe, usiwe kuhani kwangu mimi; kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako, mimi nami nitawasahau watoto wako). Utaona mahitaji ya dharura ya kuwa sehemu katika Kazi ya kusambaza maarifa haya muhimu-Ujumbe huu wa Injili ya njia ya Mungu ulimwenguni kote. Utaanza kuwa na bidii ya kufanya Kazi ya kufundisha mataifa yote njia ya amani, furaha na fahari isiyio na kifani.

Utakuwa na hamu ya KUTOA, kugawa na kusaidia ulimwengu unaoporomoka. Utaweka moyo wako wote kwenye Kazi ya Mungu. Utajitoa kabisa katika kuonya ulimwengu kuhusu matukio ya ajabu yatakayotokea kabla ya mwisho wa dahari. Baadaye utagundua kwamba hakuna kitu bora kuliko Neno la Mungu.

Ulimwengu huu umepotea katika kinamasi cha kukosa matumaini na machafuko, maporomoko na umaskini. Mtu ye yote anaye ufahamu atakubali kwamba ulimwengu huu hauwezi kuendelea zaidi. Unaweza kuwa na nafasi ya kuwambia ulimwengu wa leo kuhusu Ulimwengu wa Kesho. Ikiwa Mungu anakuita, unaweza kufurahi katika ukweli kwamba unaweza kusambaza maarifa kwa ulimwengu wote kwamba Mungu mwenyewe anaenda kuingilia kati katika masuala ya binadamu na kuokoa ulimwengu. Utakuwa na msisimko wa kuwa na nafasi ya kuwaambia ulimwengu kwamba kuna wakati ujao ulio bora-kwamba Mungu anatupenda-kwamba Mungu atatenda.

Na ukifikiri jinsi ndoa ambazo zimeenda kombo zinaweza kugeuzwa ziwe nzuri, jinsi unaweza kuwa katika nafasi ya kugeuzwa miyo ya baba iwaelekee watoto, na miyo ya watoto iwaelekee baba zao, kuziba mwanya wa kizazi hiki, kuleta uhusiano katika kitengo cha familia, na utafurahia.

Ukiwa una nafasi katika Kazi ya Mungu, utaridhika katika maarifa ya kusaidia ulimwengu jinsi ya kuwa na nyumba yenye raha, watoto wenye furaha, ndoa ya furaha na kila kitu chema na cha kutosha, maisha ya furaha. Hata utakuwa tayari kujitoa katika nafasi ya kuwasadia ulimwengu waelewe njia ya Mungu.

Ikiwa Mungu anakuita, tafadhali uelewe kuwa ya ajabu, ni kazi kubwa sana ya kuwasaidia wanadamu kuokoka kwa kujitoa kumpa ulimwengu huu

kinachotakikana sana-Njia ya Mungu,  
iongozayo kwenye maisha.

### Je Mungu Anakuita?

Ikiwa wewe, kupitia kwa (mafundisho ya CCOG, Video ya Unabii wa Habari za Biblia, vitabu,) na kurasa za jarida hili umeanza kuamini kwamba Biblia inamaanisha yanayosema-ikiwa unatambua ujumbe wa Injili kwamba ni ujumbe wa Mungu mwenyewe kwako wewe-ukiona kwamba njia zako ni mbaya-ukiwa na nia ya kusambaza na kusaidia ulimwengu huu-BASI UNAITWA NA MUNGU!

Unaitwa sasa hivi kupitia kurasa za jarida hili. Je unaenda kuitikia wito huo? Je unaenda kuitikia Roho wa Mungu na kukubali ukweli umekuwa ukipata?

Je ungependa kuishi kwa neno zima la Mungu-amini Injili na kuitikia wito kutoka kwa Mwenyezi Mungu ili uwe mionganini mwa limbuko la kwanza la Mungu?

Kumbuka, wanaoitwa na Mungu wana nafasi katika kuokoa ulimwengu huu wa vurugu. Watakuwa na nafasi ya kuhubiri ujumbe wa onyo la mwisho kwa ulimwengu huu unaozirai kabla ya mwisho wa nyakati. Watakuwa na nafasi katika kueleza Ulmwengu wa ajabu wa Kesho. Watakuwa na nafasi katika kugeuza "mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao" (Malaki 4:5-6).

Na baadaye, watakuwa na nafasi katika Ufalme wa Mungu kama wafalme na makuhani chini ya Yesu Kristo ambaye atakuwa hapa duniani akitawala mataifa yote kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.

Ni wito wa ajabu ulio nao sasa. Bila shaka Mtume Paulo alitiwa msukumo kuandika katika Waembrania 2:1-3: "Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa tusije tukayakosa.2 Kwa maana, ikiwa lile neno lililonenwa na malaika likuwa imara, na kila kosa na

uasi ulipata ujira wa haki,3 sisi je! Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza ulinennwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliosikia."


Huu wito unaendelea! Ni wito wa ajabu! Umesikia, na kusoma, na kuona. Hatua nyininge ni yako sasa!

*Kwa vile nafasi ya Kanisa la Mungu  
Ulimwenguni Kote (WCG) la zamani  
limechuliwa na shirika linalowakilisha  
sehemu ya Filadelfia ya Kanisa la Mungu,  
ungependa kuwasiliana na Kanisa la Mungu  
Linaloendelea (CCOG). Makusanyiko na  
maelezo yanaweza kupatikana kwenye  
[www.c cog.org](http://www.c cog.org)*

*Kumbuka: Ikiwa mmoja au wazazi wako wote wako katika Kanisa la Kweli la Kristo, tayari umetakaswa (1 Wakorintho 7:14) na unaitwa ikiwa utakubali wito (Mathayo 22:14; Waembrania 4:7).*

# JISOMEE KOZI YA BIBLIA

## Somo la 12b: Thibitisho la Historia ya Biblia



Bob Thiel, Mhariri Mkuu

Imechapishwa 2017 na Kanisa la  
Mungu Linaloendelea (CCOG)

Kozi hii imetokana kwa kiwango kikubwa na  
Kozi ya Mawasiliano iliyohaririwa mwaka  
1954  
iliyoanza chini ya usimamizi wa hayati  
C.  
Paul Meredith kuitia Kanisa la Mungu la  
Redio.  
Baadhi ya maeneo yake yameboreshwa ili  
yaendane na karne ya 21 (japo mengi ya  
maandishi ya awali yamebaki yalivyo).  
Kadhalika imeongezwa vifungu toka  
Maandiko  
Matakatifu, pamoja na maswali ambayo  
hayakuwemo katika Kozi ya awali.

Kumbuka: Somo hili lilikuwa refu hapo awali, ilihitajika ligawanywe katika visehemu vingi kwa vile lilikuwa refu kuliko kiwango cha toleo la jarida hili. Sehemu ingine, 12C, imepangwa kwenye toleo la jarida litakalofuata hili.

### THIBITISHO kwamba Wazee wa Biblia KWA KWELI WALIISHI

Je Ibrahimu na mababu zake kwa kweli waliishi ama maisha yao yalikuwa hekaya?

THIBITISHO gani tunalo kwamba ukoo wa Ibrahimu-Tera na Nahori, Harani, Serugi, Reu, na Pelegi-kwa hakika walikuwa MAUMBO YA HISTORIA? UTAPATA wametajwa katika Mwanzo 11.

Je wajua kinachofundishwa sana leo? Hapa ni matamko mawili ambayo yatakushangaza ikiwa una ufahamu:

“Wazee wa ngano katika MWANZO ni mashujaa wa HEKAYA waliohusiana kibandia na Israeli.” Na pia: “Kupitia kwa Musa, Yehova (Kihibrania: YAHWEH) akawa mungu wa Israeli...Yehova awali alikuwa mungu wa mlima mtakatifu (Sinai ama Horebu).” (From Langer’s *Encyclopedia of World History*.)

Leo hii nadhani wanaakiolojia wengi wanasema kwamba hakuna thibitisho la moja kwa moja la Ibrahimu, kwa mfano, ambaye aliishi. (Archeology of the Hebrew Bible. Nova, PBS, November 18, 2008)

Kweli?

Basi wacha tutathmini thibitisho zaidi.

Je Mungu ni ushirikina na hekaya ya Biblia?  
- ama Mungu ni Muumba na rekodi ya  
maandiko ni ukweli kihistoria? Moja kati ya  
dhana hizi ni UWONGO MTUPU

Gani hiyo?

1.Kwanza angalia katika BIBLIA yako na uone kwamba kwa miaka mingi imefunua kwamba watu hawa kwa ukweli walishi. Soma Mwanzo 11:18-25, na hasa mstari wa 25.

**MAELEZO:** THIBITISHO limeshangaza maelfu! Hakika ndizo hizi zilizorekodiwa miongo mingi iliyopita:

Kati ya miaka 1943 hadi 1939, uchimbuaji ulifanywa kwa utaratibu kwenye Mari ya kitambo katika ufuoni mwa Kusini magharibi ya Mto Frati Karibu na Mesopotamia ya kitambo (Iraki ya sasa).

UNADHANI WALIPATA NINI?

MIJI NA MAJIFI KATIKA MESOPOTAMIA YA KALE ILIPEWA MAJINA BAADA YA KILA MMOJA WA WAZEE WA KITAMBO!

Rekodi zilizochimbwa ya miaka 3,000 iliyopita zinaongea juu ya "Mji wa Nahori" (uliopewa jina la Nahori) ultiotajwa katika Mwanzo 24:10. Ulijengwa karibu na jiji la Harani ambao bado upo hadi leo hii! Nani alisema kwamba watu hao ni hekaya?

"Licha ya eneo dhahiri ya miji ya wazee wa Biblia ya HARANI na NAHORI linalopatikana kaskazini magharibi ya Mesopotamia, hakuna onyesho lolote la maskani ya Hibrania katika eneo hili ambalo linaonekana majina ya mababu ya Ibrahim, ambalo linalingana na majina ya miji iliyo karibu na Harani: SERUGI (Ashuru SARUGI), TERA (TIL TURAKHI, 'Boma ya Tera,' katika nyakati za Washuru)... REU pia linalingana na majina ya baadaye ya miji katika ufa wa Frati ya Kati. PELEGI, kwa mfano, ulioitwa Paliga baadaye kwenye Frati katika mdomo wa Haburi." (From Unger's "Archeology and the Old Testament")

Vibao nya Elba, ambavyo vinakaribia miaka 4000, vinataja Ibrahim na pia Sodoma na Gomora kulingana na David Noel Freedman (ona pia karatasi yake, Elba Tablets and Abraham Tradition, BYU, 1978).

Wakosoaji bado watapuuzia rekodi hizi na kudai kwamba Biblia ni hekaya. Wakati wao wa KUHESABU uko pembeni na unakaribia haraka! Biblia haidanganyi. Lakini wengi wanaoitwa wanasayansi hawawezi kugundua ukweli (1 Timotheo 6:20), hata kama u mbeleni mwao (2 Timotheo 3:7).

**Thibitisho Yusufu kwa Hakika Alikuwa Msaidizi wa Karibu wa Farao!**

Kwa miongo mingi, wenyewe shaka wamechekelea juu ya "riwaya" ya Yusufu. Kuna THIBITISHO gani kwamba Yusufu alichaguliwa kuwa mtu wa pili katika mamlaka ya Misri? Bila shaka ikiwa kulikuwako na miaka saba ya janga la njaa ya ajabu na Yusufu ndiye aliwaonya kuhusu janga hili-lazima kuweko na rekodi mahali!

1. Je Biblia yako inasema kwamba Farao aliweka Yusufu juu ya Misri yote? Mwanzo 41:41.

**MAELEZO:** Je kuna rekodi hiyo ya KIHISTORIA? Ama Biblia ni hadithi ama matokeo ya ngano ya Kiyahudi?

JIBU linapatikana katika utawala wa Amenemheti III wa Misri ambao unaitwa nasaba ya kumi na mbili. Amenemheti alichukua tabu kubwa kusoma kiwango cha Nile na akafanya kazi kubwa sana ya unyonyizaji. Alipanua nafasi ya Ziwa Moerisi katika Fayumi. Kwa ziwa ALISABABISHA mfereji mpya kutengenezwa. Mfereji huu unaitwa "BAHR YUSUF" na Wamisri. Maana ya BAHR YUSUF NI "MFEREJI WA YUSUFU"-Kwa hakika, Yusufu alisimamia ujenzi wake kwa niaba ya mfalme huyo! Miaka saba ya njaa ya kutisha ilikuwa inakaribia haraka!

Karibu na Ziwa Moerisi Mfalme alipata kujenga "Libirinthi" mkubwa. Lilikuwa ni

jingo kubwa lililotanda kwenye ekari nyingi. Lilifanya kama kikao kikuu cha serikali na kituo cha utawala ya kugawanya utoaji wa serikali na uhifadhi ya asilimia 20 ya nafaka zilizopatikana katika miaka ya mavuno (Mwanzo 41:34) ili zitumike wakati wa njaa. Kuwepo kwake na majira yake inaenda na rekodi ya Biblia ya mapendekezo ya Yusufu ya kuhifadhi <sup>1/5</sup> ya nafaka wakati wa miaka ya mavuno:

Katika karne ya 5 K.K, Herodoto aliandika kwamba Liribinthi ulikuwa "juu ya ziwa Moiris na nyuma yamji ulioitwa Mji wa Mamba" ('Histories', Book, II, 148).

**Mji wa Mamba (Crocodilopolis)** ulikuwa mji wa zamani katika Heptanomisi, kwenye ukuwa magharibi wa Nile, kati ya mto na ziwa Moerisi, kusini magharibi ya Mefisi. Kusini mwa eneo la Crocodilopolis, kwenye lango la unyogovu wa Oasizi wa Faiya, inapatikana Hawara, eneo la Akiolojia ambayo ni maskani ya piramidi ya Amenemhat III, mfalme wa mwisho wa nasaba ya kumi na mbili (K arne 1855-1808 K. K). (Holloway A. The Lost Labyrinth of ancient Egypt-Part 3: Uncovering its location. September 4, 2014).

Lakini wapi rekodi kuhusu NJAA ya miaka saba?

"Moyo wangu una wasiwasi mkubwa," alisema Mfalme Zosa wa nasaba wa III, "kwa sababu wakati wangu mto Nile haujafurika kwa muda wa MIAKA SABA. Nafaka ya konde zimekuwa haba; mimea imeshidwa kufanya vizuri, vyakula vimekosa. Kila mtu anaibia jirani... watoto wanalia, vijana wanaenda... watu wa kotini wanakosa akili ya kuongea. Gala zilijengwa lakini zilizokuwa ndani zao zimetumika zote," anaomboleza (from Barton's

"Archeology and the Bible," p. 305).

Taarifa hii inatoka kwa kinachoitwa Jiwe la njaa(Stela). Jiwe linaloitwa stele/stela ni jiwe lililosimama imara ama mnara ambao kikawaida linabeba maandiko ya kumbukumbu ama sanamu ya mchoro.



Jiwe la Njaa

Makala ya hayati Dk. Hoeh *Nani Alijenga Piramidi?* Inadai Amenemhet III (Misri ya juu) na mfalme Josa/Zosa (sehemu ya Misri ya chini) alitawala wakati wa Yusufu (Amenemhet III 1741-1692 K. K na miaka 7 ya njaa 1727 mpaka 1720 K. K). Wakati kuna utata unaohusiana na tarehe ya tukio hili, ni ya muhimu ukilinganisha na Mwanzo 41:29-32 na 47:13-27.

Mwanzo pia inarekodi kisa cha Yakobo kuingia katika Gosheni unaopatikana Misri, na Israeli kuongezeka kuwa taifa la wanaume, wake na watoto milioni 2 na nusu katika karne mbili tu. Wapi basi REKODI kwamba Israeli waliishi Misri wakati huo? Wenye shaka wanasema hamna rekodi, historia inasema kunao!

Bado tunataja kutoka kwenye "Historia ya Farao" na Weigali, juzu 2, kurasa 129-130:

Msingi wa umbo ilioandikwa jina la mfalme (yaani na jina la Amenemhet III) imepatikana Teli Yehudi, "Mlima wa Wayahudi," sehemu mbayo ni maili 20 kaskazini mashariki ya Kairo, kwenye njia inayoelekea moja kwa moja hadi "Nchi ya Gosheni," Wedi Tumilati. Inaonekana ilipatikana

wakati wa utawala wa Amenemheti III, na inavezakuwa imekaa kuanzia mwanzo wa makazi ya Waasia, ambapo kuna uwezekano WANAOHUSIANA na Yusufu walichukua makazi yao.

Kwa kweli ilikuwa! Biblia inasema hivyo! (Mistari mengine inayohusiana na nchi ya Gosheni inapatikana katika Mwanzo 45:9-10; 47:27). Hicho ni kiungo zaidi katika thibitisho la msisimko linaloonekana ya historia-thibitisho kwamba Biblia inamaanisha inayosema.

Inafaa ielezwe kwamba sababu moja ambayo inafanya wengi kukosa kugundua Yusufu (ama Musa) ni kwamba katikati ya tarehe za karne ya 13 K. K zimetajwa kama tarehe za Kutoka na wataalamu wasiofaa na ni mbali na karne 2 kwa vile wanadhani Ramesi II ndiye alikuwa Farao wakati huo. Kutoka kwa wana wa Israeli kule Misri kwa hakika ilifanyika katikati ya karne ya 15, mnamo 1446 K.K.

Kulingana na masomo mengine ya maandiko kwenye "Mernepta Stela/Jiwe la Manepta," Waisraeli wa zamani tayari walikuwa wameishi katika nchi ya Kanani mnamo 1213-1203 K.K kabla ya utawala wa Manepta (Jurgen von Beckerath, Chronologie des Pharaonischen Agypten, Maiz, (1997), pp. 190)." Jiwe la Manepta" liligunduliwa katika mwaka wa 1896. Linaonyesha vita, linaonyesha watu ambao wamevaa kama Wakanani, na inaonyesha Misri ikiharibu mazao ya Israeli. Hii mbegu inavezakuwa mimea kwa sababu Misri hawakuharibu Israeli wote wakati huo.



Jiwe la Manepta

Hata hivyo, Jiwe la Manepta kimsingi linamaanisha kwamba dhana kuwa Kutoka kulifanyika wakati wa Ramesi II haiwezekani.

Kwa nini?

Ramesi II anadaiwa kutawala mpaka 1213 K. K na Biblia inaonyesha kwamba wana wa Israeli walitangatanga kwa miaka arobaini jangwani (Hesabu 14:34-35; 32:13) kabla hawajaishi katika nchi ya Kanani. Haitakuwa na maana kwamba Ramesi II aliyeshindwa angetawala kwa kadri ya miaka 30 (Miaka 40, chini na miaka kumi ya Manepta) baada ya kukabiliana na mapigo na kupotea kwa jeshi kama ilivyoelezwa katika Kitabu cha Kutoka.

Lakini makosa ya 'wataalamu' ukiongezwa na makosa mengine wamewazuia kufundisha ukweli. Maandiko, "wakijifunza siku zote, ila wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kweli" (2 Timotheo 3:7) yanakuja kwa mawazo.

#### Mfalme Daudi Akaacha Alama Yake

Kuna nini kuhusu Mfalme Daudi?

Karibu wakosoaji wote wametia shaka sehemu ya historia ya Daudi kupanda kwa umaarufu chini ya Mfalme Sauli Mbenyamini. Ni THIBITISHO gani tunalo?

1. Je Biblia yako inasema kwamba Daudi alipata heshima ya kimataifa wakati wa umaarufu wa kabile la Benyamini? 1 Samueli 18:7,8 na 21:11.

**MAELEZO:** Kwa hakika ikiwa Daudi alikuwa mkubwa kama jenerali, heshima yake

ingesambaa mbali sana hadi Mto Frati ambaa baadaye ukawa mpaka wa Israeli.Na ikiwa kabilia la Benyamini walikuwa tawala iliyokuwa mionganii mwa Waisraeli katika mapambano dhidi ya Wafilisti, inafaa itajwe.

Ni nini ushahidi wa Kihistoria?

Hayati Dk. Herman Hoeh aliandika kwamba Akiolojia kuupuzia Mfalme Daudi ni kosa:

### Sauli na Daudi katika Akiolojia

Lakini ushahidi wa nguvu dhidi ya tafsiri ya kisasa ya akiolojia uligunduliwa na Mfaransa wa Mari kwenye Mto Frati.Hapo paligunduliwa kwamba katika maisha ya Hamurabi-ambayo ilirekodiwa na Wahistoria katika wakati wa Abrahamu-Wabenyamini walikuwa wakidhibiti Palestina na watu kama Daudi walikuwa na umaarufu! (See Werner Keller's The Bible as History, pages 49-52).

Kutoka kwa kibao kilichopatikana Mari, tunasoma maneno haya yaliyo wazi: "Mwaka ambao Landulimu alienda Heni na kuweka mikono kwenye wilaya ya Wabenyamini," na "Mwaka ambao Zimrilimu aliwa Davidam wa Benyamini."

Hakika! Chini ya Mfalme Sauli, Wabenyamini, kabilia la Benyamini walikuwa wengi. Mataifa walichukua Palestina yote kama nchi ya Wabenyamini.Na Daudi alikuwa jenerali mkubwa kuliko majenerali wote wa Benyamini (1 Samueli 18:7;21:11). Umaarufu wa Daudi ulisambaa mbali kiasi kwamba Mataifa walikuwa wakiwaita majenerali wote wa Israeli Davidam, ama "Daudi"-watu kama Daudi-kama vile Warumi Kaisari waliokuwa "wakuu" ulimwenguni waliwapa majina Kaisaria wa Ujerumani na Siza wa Urusi.

Ni jinsi gani wanahistoria na wanaakiolojia wanetafsiri uvumbuzi huu wa kushangaza? Je wangeweka wakati wa Hamurabi ulingane na wakati wa Sauli na Daudi? Siyo hivyo! Badala yake, wanapuuzia kiujanja kwamba Wabenyamini walikuwa Palestina muda mrefu kabla ya Benyamini kuzaliwa-kwamba jina Daudi lilikuwa na umaarufu kwa kadri miaka elfu kabla ya Daudi kuzaliwa! Walitumai kutunza tafsiri zao za orodha ya wafalme na kukataa Biblia.Maelezo ya wanadamu yalitumika kuepuka MAMLAKA ambayo yamewekwa katika sheria ya Biblia! (Archeology proves the Bible plain! Plain truth, September 1963, p.47)

Hapa ndipo Wabenyamini wametajwa na majenerali wao wameitwa "DAVIDAMI" ama DAUDI! Mfalme Sauli alikuwa Mbenyamini (1 Samueli 9:21) na alikuwa amemfanya Daudi kusimamia viongozi wa jeshi lake (1 Samueli 18:5).

Kama vile Warumi "wakubwa" waiotwao KAISARI waliwapa jina kwa KAISA wa Ujerumani na Zisa wa Urusi, kwa hivyo umaarufu wa Daudi ulisambaa mbali sana hadi Mataifa wakawaita Wakubwa na majenerali wa Israeli "Daudi"-watu kama Daudi! Na umaarufu wa Benyamini ulisambaa kwa muda na kabilia hilo wakawapa Israeli wote jina kama vile Efraimu na Yuda walivyofanya baadaye.

Ni jinsi gani wakosoaji wa Biblia wanapata rekodi wazi ya historia katika siku ya Daudi? Kwa kusema kwamba Wabenyamini walikuwa katika Palestina kusini magharibi ya Frati kabla ya Benyamini kuzaliwa-na miaka 750 kabla Daudi kuishi kulikuwako na majenerali walioongoza ambao walikuwa na jina "Daudi."

LAKINI TAFSIRI YAO MBAYA YA HISTORIA HAITASIMAMA, kwa sababu rekodi ya wakati huo ina maelezo kwamba "Yahweh

ni Mungu.” Mungu ALIJITAMBUA mwenyewe na jina “YAHWEH” ama “Mungu wa Milele” ama “Bwana” kwa wakati wa kutoka (Kutoka 6:3). Mataifa wangejua jina lake kwa kupitia tu kwa mawasiliano na Israeli, na kwa wakati Waisraeli walikuwa wakipanuka kwenda Mto Frati kuelekea Mari! Na ilikuwa lini? -KATIKA SIKU YA SAULI NA DAUDI! (soma 2 Samueli 8:3-10).

Inafaa pia ikumbukwe kwamba maandiko “Nyumba ya Daudi” ilipatikana Tel Dan



stele/Jiwe la Tel Dani (karne ya 9 K. K). Na Mesha Stele/Jiwe la Mesha (karne ya 9 K. K) (Wood BW.The Tel Dan Stela and the Kings of Aram and Israeli for Biblical Research, May 4, 2011).

#### *Jiwe la Tel Dani*

Hili ni thibitisho kwamba Biblia ina ukweli na ‘wataalamu’ wana makosa.

Mara nyingi, wasomi, katika ‘maarifa’ yao ya kibinadamu wamejaribu kutoa sababu nyingi ya nje ya uthibitisho ulio wazi na rahisi ya historia ili wapate kuharibu rekodi iliyo na mamlaka ya Neno takatifu la Mungu!

#### **Danieli Alithibitishwa!**

Pengine Kitabu kilichopingwa sana katika Biblia ni Danieli.Wakosoaji wameweka maandiko yake miaka 400 baada ya wakati ufao wa Danieli.Wakosoaji wengine wamedai kwamba ni ya kughushi,

kinachojificha katika jina Danieli (ambao kuwepo kwake pia wana shaka nako!)

Unapaswa kujua aina ya udanganyifu wasomi wa ulimwengu huu wamewekeea Biblia.Akisema Dereva, ASIYEAMINI, katika kitabu chake “Utafiti wa Kisasa unavyooleza Biblia”:

“HAKUNA MAZINGIWA wa Babeli na Koreshi...aliingia huku bila pigo...maelezo ya Herodota...ya maji ya Frati ambayo yaligeuzwa na Koreshi na majeshi yake kuingia wakati wakaaji walikuwa akishereka, ni riwaya; ...Belshaza pia hakuwa mfalme wa Babeli...na hata hakuna nafasi ya “Dario wa Medi’ kuwa mfalme wa Babeli.”

Hii ndio taaluma ya upuuzi wengine wanafundisha. Biblia inasema UKWELI kuhusu kuanguka kwa Babeli.Wacha tutahmini!

1.Je Danieli 5:24-30 inasema kwamba mflame wa Wakaldayo-Wababeli-akauawa na ufalme wake kuuchukuliwa? Na ufalme huu ulioshindwa baadaye ultoka kwa Dario, Mmedi, hadi Koreshi? Danieli 6:28.

**MAELEZO:** Haya ni ukweli, kwa utaratibu vile ulifanyika, na ultunzwa katika maandiko ya Senofoni.

Senofoni, mwana historia kutoka Ugiriki aliyeandika “Kiropedia” katika karne ya nne kabla ya Kristo, akisema kwamba:

“Wakati walifika Babeli” mnamo 539 K.K alichimba mitaro ya maji ya kupeleka maji katika Mto Frato ambayo yalikienda chini ya malango ya Babeli Alafu yeye na jeshi la Wamedi-Wajemi walienda chini ya maji ya mto kisiri, wakapanda polepole kupitia malango kwenye Mto na wakikimbia kwa ikulu “wakati alisikia ya kwamba kuna karamu katika Babeli, ambapo Wababeli walikunywa na kupiga kelele usiku kucha.” Alipofika

mahali ambapo Belshaza aliona maandiko kwenye ukuta, waliingia ndani na kufuutilia wale amba walikimbia, na kuwapiga, wakaja kwa mfalme wakampata akisimama na kisu chake ki tayari... wakamdunga.”

#### KWA HIVYO BELSHAZA MFALME WA BABELI ALIUWAWA USIKU HUO KAMA VILE DANIELI ALISEMA.

Baadaye wakati amani iliregeshwu, Koreshi alikuwa na hamu ya kuona baba yake hapo Uajemi. “Lini,” aliandika Senofoni, “walikuja Medi, Koreshi aligeuka na kumtembelea mjomba wake Sisari. Baada ya kumbatiana, Koreshi kwanza alimwambia Sisari kwamba kulikuwa na chumba rasmi na kasri ambazo zilitengwa kwa ajili yake kule Babeli; ya kwamba wakati atakapoenda”-wakati Sisari atakapoenda Babeli- “anaweza kulala na kupumzika nyumbani mwake.”

Nani huyu alikuwa anaitwa Sisari? Anaaminika kuwa yule aliyeitwa DARIO Mmedi! DARIO Mmedi, mjomba wa Koreshi, “alipokea ufalme” wakati Koreshi alienda kuona baba yake.

Historia tena inathibitisha Biblia kama Ukweli. Dario Mmedi Alipokea ufalme kutoka kwa Koreshi. Ilikuwa wakati Koreshi alikuwa na baba yake huko Uajemi ambapo mjomba wake Dario aliwekwa KWA MUDA kuwa mfalme juu ya milki wa Wakaldayo”! (Danieli 9:1).

#### THIBITISHO kwamba Yesu Mnazareti ALIISHI!

Watu wengi wanachukua kuwepo kwa Yesu Mnazareti kama upuzi tu. Hawajawahi KUTHIBITISHA kama rekodi ya Yesu katika Agano Jipywa KWA HAKIKA ni ukweli! Je umewahi KUTHIBITISHA kama Yesu aliishi?

Miongo mingine iliyopita, watu walikabiliwa na kitabu cha ajabu kilichokuwa na mada “Yesu-Mungu, Mtu ama hadithi?” na aliyejiri ukafiri, Herbert

Cutner. Kulingana na mchapishaji, kitabu hiki ni:

“matokea ya utafiti kwa upana na thibitisho kwamba Yesu hajawahi kuishi. Mhusika wa Biblia asiyejulikana na historia Yesu amesimamishwa,” anadai mchapishaji, “Kwa ukweli uliochujwa kimakini amba utashangaza wale amba wamempa mada hii mawazo kidogo. Mkusanyiko wa ushahidi kwamba Yesu ni mhusika wa KUVUMBULIWA,” akitamatisha maandiko haya, “ hiki kitabu kimetolewa na nguvu ya kusema kwamba Yesu, mtu aliyeenda pande zote ‘akitenda mema’ hakuwa ...mtu mwenye nyama na damu...”

Haya ni maelezo ya kinukuu! Lakini je ni nini kuhusu thibitisho? Ni jinsi gani wakafiri na wakosoaji wamekuwa WAAMINIFU na ukweli wa historia?

Ikiwa ukweli wa historia unathibitisha kuwa Yesu aliishi, ikiwa watu walioishi wakati wake na maadui wake wanatoa ushahidi wa ujumbe wake na miujiza yake-basi hakuna mkafiri, hakuna mkanaji, hakuna mwenye shaka wa kisasa anaye kisingizio!

Kuna THIBITISHO GANI, NJE YA BIBLIA, kwamba Yesu aliishi? Kwamba alifanya miujiza? Kwamba aliletä Habari Njema-Injili-ulimwengu? Kwamba aliteswa na akauawa chini ya Mtawala wa Rumi Pilato? Na alichagua mitume? Kuna THIBITISHO GANI kwamba alizaliwa na Bikra mdogo?

Biblia, hakika, inasema kweli hizi. Lakini je twaweza KUAMINI Biblia? Ni thibitisho gani NJE ya Biblia yenyewe upo kwamba Yesu alikuwa umbo la kihistoria? Kwa watu wote Wayahudi wote wanapaswa kujuah? Wacha tuone.

1. Je Biblia inatuonyesha kwamba Kristo alikuwepo? MATHAYO 1:16,18,21;2:1;27:37.

**MAELEZO:** Kuna rekodi nyingi za awali zinazoonyesha kwamba Yesu alikuwepo kuliko mtu ye yote katika ulimwengu wa zamani.

Na bado “wataalamu” wengine wanakataa kukubali ushahidi.

Kwa hakika, ikiwa Yesu hakuwepo, Wayahudi hawangekuwa na sababu ya kumkana! **HATA KAMA WAYAHUDI HAWAKUMPENDA YESU, WALILAZIMISHWA NA HALI YA NGUVU ZAKE WAKAMTAMBULISHA KATIKA REKODI ZAO.**

**REKODI** ya Wayahudi inasema nini?

Ni nini wakafiri wanapuuzia kimakusudi wakati wanajifanya kukataa ukweli wa Yesu Kristo?

Yesu mara nyingi anatajwa katika Talmudi ya Wayahudi! Talmudi ni rekodi ya midahalo, mafundisho, hadithi na desturi zilizotunzwa kuanzia wakati kabla ya Yesu kuzaliwa hadi karne ambazo zinafuata kuzaliwa kwake. Kumbukumbu hizi zimejulikana kwa undani na wasomi wengi. Yesu Kristo hajatajwa na jina, ila tu mara moja ama mara mbili, mahali alisemekana kuwa mwabudu sanamu aliyeabudu kipande cha tofali (sanh.,107B). Anaitwa kimadharau “mtu huyo” ama “Mwana wa Namiri,” ama “mbwa mfu,” aliyening’inizwa, “mchawi,” “Balaamu,” na “Mtongozaji.”

Kamusi Elezo ya Wayahudi inaorodhesha mahali ambapo Yesu ametajwa katika Talmudi.Kamusi hii inataja kama “hila” tu ya kujaribu kwa wakafiri kuepa maelezo haya ambayo yanahu Yesu Mnazareti.

Yesu wakati mwingine anaitwa katika Talmudi, “Mwana wa Namiri” kuficha kweli kwamba alizaliwa na Bikra mdogo! Vifungu viwili vya enzi ya kitalmudi ambavyo vinamhusu Yesu kama mwana wa Namiri/Pantera ni: “Yakobo...alikuja kumponya katika jina la Yesu mwana wa Namiri” (Tosefta Hullin 2:22ikiendelea) na “Yakobo...alikuja kumponya katika jina la

Yesu mwana wa Namiri” (QoheletRabbah 1:8(3)).

Pandera ni neno ambalo linamaanisha Namiri au chui- (neno liundwalo kwa kubadilisha herufi za neno jingine) kwa neno la Kigiriki ni “parthenos” maanake “bikira”! Wayahudi walibadilisha kuzaliwa kwa Yesu na bikra ili ionekane kwamba alikuwa kimaumbo mwana wa Namiri ama chui! -kwa sababu vile neno “panther” ni NAMIRI ambalo Wayahudi walichafua na nahau ya Kiyahudi PANDERA.

Hizo ni kumbukumbu kwa kuzaliwa kwake Yesu na bikra! Lakini wanatheolojia wa kisasa kama vile wakanaji na wakafiri wanasisitiza katika kukataa hiso!

Miujiza ya Yesu haikukanwa na Wayahudi.**BADALA YAKE, WAYAHUDI WALIOMWONA YESU AKIFANYA MIUJIZA HIO WALISEMA ALIJIFUNZA UCHAWI KULE MISRI-**ambayo pia ni njia nyingine ya kukubali tunachokisoma katika Mathayo 12:24:

Lakini Mafarisayo waliposikia, walisema, Huyu hatoi pepo, ila kwa Beelzebuli mkuu wa pepo.

Talmudi inarekodi mahali Yesu aliponya kipofu, aliyejeruhiwa, mwenye ukoma. Pia inataja vile alitembea juu ya bahari! Pia kuna orodha kamili ya kumbukumbu ya mamake Yesu, bikira Mariamu.Matukio haya kwa hivyo YANATHIBITISHA hapa kuwa UKWELI wa kihistoria-zilirekodiwa na maadui hasa ya Yesu!

Yesu siyo kwamba aliishi peke yake lakini Wayahudi katika Talmudi ni mashahidi wa miujiza yake! Wacha wakafiri wasiojua wakatae hayo!

Talmudi kwa hila inaita injili ambayo Yesu alihubiri kama “avengil,” maanake “karatasi nyekundu.” Hawakutaka kutumia neno la awali “evangel,” linalomaanisha habari njema. Hawakupenda habari njema ya Ufalme ilioletwa na Yesu.Hawakutaka Ufalme wa

Mungu kuwatawala-kuwaambia  
wanachotakikana kufanya!

Haya ni baadhi ya matamko kuhusu Yesu  
kutoka vyanzo nya Wayahudi:

### **Maelezo mafupi kutoka Historia ya Kanisa ya Agapi (wa Arabu)**

Kwa wakati huo kuna mtu mwenye hekima  
aliyekuwa akitwa Yesu.Na matendo yake  
yalikuwa mema na alijulikana kuwa  
mwadilifu. Na wengi kutoka mionganini mwa  
Wayahudi na mataifa mengine walikuwa  
wanafunzi wake. Pilato alimhukumu  
asulubiwe na kumwua. Na waliokuwa  
wanafunzi wake hawakuacha kuwa  
mitume. Waliripoti kwamba aliwatokezea  
siku tatu baada ya kusulubiwa na akawa  
hai tena. Kulingana na hayo pengine  
alikuwa Masihi kulingana na manabii  
ambao walitabiri ajabu.

### **Talmudi ya Kibabeli**

Katika siku moja ya Pasaka Yeshua  
alisulubiwa. Siku arobaini kabla ya  
utekelezaji huu mbiu ilipigwa na ikalia  
hivi, "Anaenda kupigwa mawe kwa sababu  
amekuwa akifanya uchawi na aliwashawisi  
Israeli kwa upotofu. Ye yote atakayesema  
neno la kumwonea huruma, wacha aje  
mbele na atetee kwa niaba yake." Lakini  
kwa vile hakuna neno lililetwa ya  
kumtetea alisulubiwa katika siku ya  
Pasaka.Sanhedrini 43a.

Yeshua ni jina la kawaida Jesus katika  
Kizungu.

Sasa kuna kazi ya sanaa ya Kiyahudi isiyo  
ya kawaida ambayo pengine inapaswa  
kutajwa.



*Jiwe la Yeselisoni*

Kazi ya sanaa hii imekuwa ikiitwa Ufunuo  
wa Gabrieli, Hazoni Gabrieli (Njozi ya  
Gabrieli), ama Jiwe la Yeselisoni.Pia  
imeelezwa kama "Kitabu cha Bahari Mfu  
kwenye Jiwe." Ni jiwe la futi tatu kwa  
urefu (Mita moja) kibao cha mistari 87 ya  
maandishi ya Waebrania kilichoandikwa  
katika wino, kinachobeba mkusanyiko wa  
unabii mfupi mfupi ulioandikwa katika mtu  
mmoja na umerejelewa hadi mwisho wa  
karne ya kwanza K.K.

Kimsingi, ina madai kwamba Gabrieli  
anasema kwamba "Mfalme wa wafalme"  
atafufuka baada ya siku tatu. Wengine  
wameamini kwamba hii inaonyesha kuwa  
Wayahudi wangeelewa kuhusu kufufuka  
kwa Yesu kabla kuzaliwa kwake kwa hivyo  
dhana ya ufufuo haikuwa kitu kigeni katika  
Uyahudi (K. v. Broner E. Ancient Tablet  
Ignites Debate on Messiah and  
Resurrection. New York Times, July  
6,2008).

2.Je maandiko yanafunua mitume wa  
Kristo? Mathayo 10:1-12.

**MAELEZO:** Yusufu, Myahudi asiyekuwa  
Mkristo MWANAHISTORIA wa karne ya  
kwanza, pia anakubali historia ya Yesu na  
wanafunzi wake, kama vile anavyofanya  
pia Yohana Mbatizaji.Anamwita Yohana  
Mbatizaji "Mtu mwema" (Nyaraka za  
Wayahudi, iviii:5,2). Wasomi wanatambua  
ukweli wa maelezo ya Yusufu kuhusu kifo  
cha Jakobo, "ndugu wa Yesu aliyeitwa  
Kristo" (Ant., xx:9,1).

Hizi ni dondo mbili kamili kutoka kwa  
Mwanahistoria Myahudi Yusufu (karne ya  
kwanza):

**Nyaraka 18.3.3** Wakati huo kulikuwako Yesu, mtu mwenye hekima, ikiwezekana kisheria anaweza kuitwa mtu, kwa sababu alikuwa akitenda mambo ya ajabu, mwalimu wa wale watu walioupokea ukweli kwa furaha. Aliweza kuvuta Wayahudi wengi kwake, na watu wa mataifa mengi. Alikuwa Kristo, na wakati Pilato, kwa pendekeso la watu wakuu mionganoni mwetu walimhukumu kwa msalaba, wale waliompenda tokea mwanzo hawakumwacha, kwa sababu aliwatokezea tena baada ya siku tatu; kama vile manabii walivyotabiri haya na mambo mengine elfu ya maajabu yaliyotabiriwa kumhusu.

**Nyaraka 20.9.1** Lakini kijana Anana ambaye kama vile tulivyosema, alikaribisha kuhani mkuu, alikuwa na msimamo thabiti na ya kipekee; akafuata chama cha Wasadukayo, ambao walikuwa wakali katika hukumu kuliko Wayahudi wote, kama vile tumekwisha kuonyesha. Kwa vile Anana alikuwa mtu wa msimamo, alidhani kwamba ana nafasi nzuri, baada ya kifo cha Festo, na Albina bado alikuwa katika njia; kwa hivyo aliwakusanya baraza ya hakimu, na akaleta mbele yao ndugu ya Yesu, aliyejulikana kama Kristo, yaani Jakobo, pamoja na wengine, na baada ya kuwashtaki kama wavunja sheria, akawakabidhi ili wapigwe mawe.

Je Warumi walijua kwamba punto Pilato alitoa hukumu ya kusulubiwa kwa Yesu? Alisema Cornelio Tasito mnamo 115 B.K., katika Kumbukumbu yao, XV, 44:

**Kumbukumbu.**  
**15,44...**Wakristo...Kristo, mwanzilishi wa jina hili, aliuawa na Ponto Pilato, mhukumu wa Yuda

katika utawala wa Tiberio. Lakini ushirikina wa uharibifu ulikoma kwa muda, uliletwa tena, sio kuptia kwa Yuda pekee ambapo uharibifu huu ulianzia... (Annals of Tacitus. As cited in Giles JA. Heathen records to the Jewish scripture history: containing all the extracts from the Greek and Latin writers, in which the Jews and Christians. James Cornish, 1856, p.105)

Kwa hivyo, vyanzo vyta kawaida kutoka kwa wale ambao hawakudai kuamini Yesu walirepoti kumhusu:

Hii ni dondo Kutoka Sutonio. Anaeleza kwamba mnamo 49 B.K., Mtawala wa Rumi Klaodio aliwafukuza Wayahudi wote kutoka Jiji la Rumi (Hili pia linafanana na tukio lililotajwa katika Matendo 18:2):

“Aliwafukuza Warumi kutoka Rumi, wakati kulikuwako na ghasia kila mara, uchochezi ulioletwa na Kresto” (Maisha ya Wakaisaria, Bk. V, 25).

*Kresto* ni neno la mtaani na la madharau linaloashiria Kristo. Sustoni hakuwa Mkristo na alitaja Wakristo kama watu wanaoshikilia “Riwaya ya ushirikana wa kifedhuli” (*Life of Nero*, 16.2, as cited in Bock DL. Studying the Historical Jesus: A Guide to Sources and Methods. Baker Academic, 2002, p. 48).

Kuna THIBITISHO Yesu aliishi!

Haya hayakuwa maandiko ya Mkristo, lakini mwanahistoria wa kipagani wa Rumi ambaye alichukia chochote kiitwacho Ukristo! Tasito alikuwa na fursa ya kufikia rekodi za serikali. Alikuwa na THIBITISHO kwamba Kristo alisulubiwa!

Katika karne ya 21, kitu kiitwacho James' Ossuary kilitangazwa kwa ulimwengu (ossuary ni sanduku la chaki ambalo lilitumika kubeba mifupa ya wafu. Sanduku hili lilidaiwa kuwa ni la kuanzia karne ya 1.



### *James Ossuary*

Linabeba maandiko ya Kiarama ya kuvutia:

Ya'akov bar Yosef akhui di  
Yeshua  
Hili linaweza kutafsiriwa kama Jakob (ama  
Yakobo), mwana wa Yusufu, ndugu wa  
Yesu."Wakati tarehe ya maandiko haya ni  
vigumu kuthibitisha, kifaa hiki, ni ya  
hakika, ni wazi kwamba Yesu alikuwepo na  
alikuwa na ndugu zaidi ya mmoja.

Yakobo (Ya'akov) ametajwa katika maelezo  
ya Injili kama ndugu wa Yesu (Mathayo  
Zingatia pia alichoaandika Mtume Petro:

15 Walakini nitajitahidi, kwamba  
kila wakati baada ya kufariki  
kwangu mpate kuyakumbuka  
mambo hayo.16 Maana hatukufuata  
hadithi zilizotungwa kwa werevu,  
tulipowajulisha ninyi nguvu zake  
Bwana wetu Yesu Kristo na kuja  
kwake; bali tulikuwa tumeuona  
wenye ukuu wake. ( 2 Petro  
1:15-16)

Biblia ni Ukweli na akiolojia inayofaa  
inakubaliana nayo. Hatufuati ngano za  
ujanja

13:55). Kitabu cha Matendo kinaonyesha  
kwamba wakati mmoja alikuwa kiongozi  
wa Kanisa la Yerusalem na msimamizi wa  
baraza ya Yerusalem katika Matendo 15.  
Yakobo pia aliandika kitabu cha  
Yakobo.Yeye pia amejadiliwa sana katika  
maandiko ya Yusufu.

KUNA THIBITISHO NJE YA BIBLIA-USHAHIDI  
KWAMBA YESU ALIZALIWA NA BIKRA-  
KWAMBA MIUJIZA YAKE YALITENDEKA-  
KWAMBA ALIHUBIRI INJILI YA UFALME WA  
MUNGU-KWAMBA ALIWAITA WANAFUNZI-  
KWAMBA ALIKUWA NA NDUGU ZAKE!

Ukweli NJE YA BIBLIA umerekodiwa na  
wanahistoria wasio Wakristo walioishi  
wakati wake. Zinasimama kama thibitisho  
lisilopingika kwamba mtu huyu Yesu Kristo  
Si hekaya na kwamba rekodi ya Agano  
Jipya ni UKWELI!

Kuitekeleza Mathayo 24:14  
Pamoja na  
Mathayo 28:19-20

*Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG)*  
[:www.c cog.org](http://www.c cog.org)  
*Taarifa za Unabii wa Habari za kila siku:*  
[www.cogwriter.com](http://www.cogwriter.com)



**CCOG.ASIA:**Hii ni Tovuti ilengayo wasomaji kutoka Asia.Inazo makala katika lugha ia Kichina ya Mandarin pia katika Kiingereza pamoja na lugha zingine za Kiasia.

**CCOG.EU:**Hii ni Tovuti kwa wale wa Ulaya.Inazo makala katika lugha za Ulaya.

**CCOG.IN:**Hii ni Tovuti inayolenga walio wa asili ya Kihindi.

**CCOG.NZ:**Hii ni Tovuti ilengayo walio wa asili ya New Zealand.

**CCOGCANADA.CA:**Hii ni Tovuti ilengayo walio wa asili ya Canada.

**CDLIDD.ES:**Hili ni Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) katika lugha ya Kihispania.

**PNIND.PH:**Hii ni Tovuti kwa ajili ya wale wa Ufilipino ama wenye asili yao.



**Chaneli ya Habari za Unabii wa Biblia:**  
[www.youtube.com/BibleNewsProphecy](http://www.youtube.com/BibleNewsProphecy)  
**Chaneli ya Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG)**  
[:www.youtube.com/continuingcog](http://www.youtube.com/continuingcog)

Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) pia hutumia majarida na magazeti ya kielektroniki,vitabu na barua za kila Juma kwa waumini wake katika kuitekeleza Mathayo 24:14 na Mathayo 28:19-20.

